**TUNDU** Lissu atua nchini Kenya kwa shughuli maalum

UKURASA 3



**WADAU** tasnia ya habari wamlilia Mkinga Mkinga

UKURASA 3




NEEMA NDANI YA WIKI YA UTUMISHI...

**REA yaanza Mtwara Awamu Tatu kuneemesha umeme kwa vijiji 300**



UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Juni 25, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580622

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# Tanzania na WHO kuteta corona III

**SERIKALI** yakiri kuandika barua kuomba chanjo... *Endelea Ukurasa wa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza kikao cha Baraza la Mawaziri Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Wabunge waikaba koo serikali faini bodaboda


UKURASA 2



UKURASA WA 5

**MABADILIKO SERA, SHERIA KUTOMWACHA NYUMA MWANAFUNZI ALIYEPATA UJAUZITO**

SERIKALI imesema inatarajia kupitia...



UKURASA WA 5

**KUNYIMWA UNYUMBA CHANZO UTITIRI TALAKA**

BAADHI ya wanaume wa Kata ya Wendele, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama...

## RAIS SAMIA KUTETA NA MAASKOFU KATOLIKI

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA SAIZI YETU - BIASHARA** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

# Serikali yabanwa faini bodaboda

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WABUNGE wameibana serikali, wakiitaka ipitie upya uamuzi wa kushusha faini ya waendesha pikipiki, maarufu kama bodaboda na bajaj, kutoka Sh. 30,000 hadi Sh. 10,000.

Wamedai kuwa uamuzi huo una upungufu, hivyo utaongeza vifo na majeruhi kwa makosa ya usalama barabarani.

Wakati wabunge wakiibana serikali, Waziri wa Fedha na Mpango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema serikali italiangalia upya suala hilo kama ilivyoshauriwa kwa kuangalia hali halisi.

Baadhi ya wabunge, wakichangia Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2021/22 jana, walisema kiwango ni kidogo, hivyo kitaongeza mzigo kwa serikali na Watanzania. Pia kitasababisha ongezeko la wodi za majeruhi wa pikipiki na bajaj katika hospitali za rufani za kanda, mikoa na wilaya.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Lugangira, akichangia muswada huo uliowasilishwa juzi jijini hapa na Dk. Nchemba, alisema serikali haipaswi kuiacha faini hiyo peke yake ili kumfanya aliyefanya kosa ajifunze, na kufanya wengine wasifanye kosa na kuzua mtu asifanye kosa.

"Sasa kwa kupunguza adhabu kushuka kutoka 30,000 hadi 10,000, tunafifisha malengo ya faini. Ningependa kupendekeza kwa serikali ije na mfumo wa kuweka 'point system' kwenye hizi leseni kwamba huyu mwendesha bodaboda au bajaji, akifanya kosa la kwanza atalipa Sh. 10,000, akifanya kosa la pili atalipa faini ya Sh. 30,000.

Mbunge wa Musoma Mjini (CCM), Vedastus Manyinyi, alisema bodaboda wengi wamefurahi kuona kwamba wamepunguziwa adhabu lakini ni ukweli usiopingika kila jambo lina pande mbili, lina faida na hasara.

"Wakati fulani hivi wabunge utaona tunalalamika kwamba tunapotoa mawazo yetu serikali wakati mwingine inayapuuza. Na ni ukweli usiopingika kwamba mbunge anapokuwa anatoa mawazo huwa anaamini hayo mawazo yake ni sahihi.

"Lakini juzi, nakumbuka katika mchango wangu nilisema kwamba hawa bodaboda hawa wanalipa faini ya 30,000 na wakaendelea kufanya kosa. Bodaboda huyo anabeba abiria mmoja, dereva anayebeba abiria 60 kwa maana ya gari kubwa analipa faini ya Sh.60, 000," alisema.

Mbunge wa Geita Mjini (CCM), Costantine Kanyasu, akitoa mchango wake kuhusu jambo hilo, alisema wengi wanasema pikipiki inabeba mtu mmoja, lakini ukweli ni kwamba pikipiki anazokutana nazo barabarani zinabeba watu wanne, watano.

Kwa mujibu wa Kanyasu, inawezekana uamuzi huo wa kupunguza faini kwa bodaboda na bajaji usiposimamiwa vizuri, kama taifa tutatengeneza wodi 10 za majeruhi Hospitali ya Rufani ya Bugando na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

"Nimewahi kushuhudia pikipiki imeua watu watano iliingia kwenye trekta ikaua dereva wa pikipiki na abiria wake wote. Sasa hapa tunazungumzia mtu mmoja lakini nadhani kuna haja ya kusimamia sheria ili kuwafanya madereva wa pikipiki kuheshimu punguzo la faini lakini sheria," alieleza Waziri Mwigulu.

**MAJIBU YA MWIGULU**

Akihitimisha hoja yake kuhusu muswada huo, Dk. Nchemba alisema maoni mapya aliyoyatoa Lugangira kuhusu bodaboda, ameyapokea na atazungumza na Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, kuangalia si tu kwa bodaboda, ila kwa vyombo vyote vya moto.

"Tutaiangalia ili kuona utekelezaji wake, hata huo utaratibu unaopendekezwa wa kutumia pointi, zipo nchi ambazo zinatumia utaratibu wa aina hiyo. Lakini hili la kusema faini kupungua kutoka 30,000 mpaka 10,000 kwamba vifo vitaongezeka, kwa mtu yeyote akisikiliza hiyo hoja lazima aone kama kesho tutakuwa na shida kubwa sana," alisema.

# Samia kukutana na TEC leo Dar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kukutana na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) leo jijini Dar es Salaam.

Kuwapo kwa mkutano huo kulithibitishwa jana na Idara ya Habari (MAELEZO).

Mkutano huo ni mwendelezo wa Rais Samia kukutana na makundi mbalimbali tangu alipoapishwa kushika madaraka hayo makubwa Machi 19, mwaka huu.

Tayari Rais Samia ameshakutana na wazee (Dar es Salaam), kinamama (Dodoma) na vijana (Mwanza).

Jumapili ijayo, katika kuadhimisha Siku 100 za uongozi wake, Rais Samia anatarajiwa kukutana na wahariri wa vyombo vya habari Ikulu jijini Dar es Salaam.




Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), William Ole Nasha, akifungua Mkutano Mkuu wa 62 wa Mwaka na Mkutano wa Kiwango cha Juu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tanzania, WHO kuteta corona III

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezindua Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Sekta ya Afya (2021-2025), unaotarajiwa kutumia Sh. trilioni 47 huku ikiweka wazi kwamba kuanzia mwezi ujao itaanza vikao vya kitaalamu na Shirika la Afya Duniani (WHO) namna ya kukabili corona.

Mpango huo ulizinduliwa jana na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, jijini hapa, akibainisha kuwa kwa mwaka utahitaji Sh. trilioni 9.4.

Alisema katika kukabiliana na wimbi la tatu la mlipuko wa ugonjwa huo Mwezi Julai, mwaka huu, serikali itahusisha vikao vya kitaalamu chini ya Uenyekiti wa Mganga Mkuu wa Serikali na Uenyekiti mwenza wa Mwakilishi Mkazi wa WHO.

"Sambamba na kuanza vikao hivyo ninaelekeza vikao vya kila mhimili katika Mpango wa Taifa wa Udhibiti Ugonjwa wa UVIKO-19 vianze kwa lengo la kudhibiti ugonjwa huo nchini.

"Kama mnavyofahamu Rais Samia Suluhu Hassan aliteua kamati maalum ya wataalamu kumshauri na kutoa mapendekezo ya kukabiliana na ugonjwa huu nchini.

"Kamati ilishawasilisha taarifa na mpango kazi wa mapendekezo 19 yanayotakiwa kufanyiwa kazi na serikali," alisema.

Waziri alisema wizara yake inaandaa andiko litakalowasilishwa kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri na pia serikali imekwishaandaa andiko la kupata chanjo za ugonjwa huo kupitia Covax Facility.

Alibainisha kuwa hatua hiyo ni miongoni maeneo matano ya kimkakati katika mpango huo ya kuimarisha utayari wa kujiandaa na kukabiliana na magonjwa ya milipuko na dharura.

"Serikali itaendelea kuboresha mfumo wa kutoa taarifa ya viashiria hatarishi, ushirikishwaji wa jamii, usafi wa mazingira, udhibiti wa taka hatarishi, upatikanaji wa fedha, uratibu, mabadiliko chanya ya tabia, ushirikishwaji wa sekta nyingine, uboreshaji wa miundombinu na upatikanaji wa bidhaa muhimu na kuwajengea uwezo wataalamu," alisema.

Alitaja eneo lingine la mpango huo ni kuboresha utoaji wa huduma za afya kulingana na mahitaji ambapo serikali ya awamu ya sita itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa kuendelea kujenga miundombinu, kuongeza watumishi, vifaa tiba, dawa na vitendanishi.

Alisema eneo la tatu ni kuboresha kitita cha huduma za afya katika ngazi msingi na huduma za rufani na za kibingwa ambazo zitapelekwa kwenye hospitali zote za rufani za mikoa.

"Eneo la nne kimkakati litahusu kuimarisha uhusiano wenye matokeo chanya wa kiutendaji wa mifumo ya afya katika kuongeza wigo wa huduma, uboreshaji wa huduma za kiuchunguzi, damu salama na bidhaa kumlinda mlaji," alisema.

Waziri Gwajima alisema eneo la tano litahusu kuendelea kuwekeza katika kuimarisha mifumo ya afya hususani rasilimali watu katika sekta ya afya, dawa na bidhaa za afya, miundombinu, TEHAMA, utafiti katika sekta hiyo na serikali ya awamu ya sita imedhamiria kuimarisha Mifuko ya Taifa ya Bima ya Afya ili kufikia lengo la bima ya afya kwa wote.

Alisema katika kutekeleza mikakati na afua zilizoainishwa kwenye mpango huo, sekta hiyo imejipanga kufanikisha hilo kupitia mifumo ya kitaasisi yenye uhusiano unaolenga kupata matokeo chanya yanayotegemeana kiutendaji.

Alifafanua kuwa kiasi hicho cha fedha kinatarajiwa kuokoa maisha ya wananchi 200,000 watakaofikiwa na huduma zilizoboreshwa na wastani wa watu 400,000 watapona kwa kuwa na afya bora.

Alitoa rai kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuendelea kuipa kipaumbele sekta ya afya kutoka kwenye vyanzo vya ndani huku akiwaomba washirika wa maendeleo kuchangia rasilimali fedha kupitia bajeti kuu ya serikali, mfuko wa afya wa pamoja na programu za kimkakati zenye lengo la kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Pia, aliomba Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuendelea kutoa vibali vya ajira ili kuziba nafasi wazi zilizoko kwenye sekta ya afya pamoja na miundombinu mipya iliyojengwa na serikali.

Akizungumza kwa niaba ya wadau wa maendeleo wa sekta ya afya, Mkurugenzi Mkazi wa USAID Tanzania, Andrew Karas, alisema wanaamini utekelezaji wa mpango huo kwa wakati utafanikisha malengo ya sekta ya afya.

Alisema wadau hao wataendelea kuiunga mkono serikali ili kufikia malengo hayo.

Waziri Gwajima alisema mapitio ya mpango uliopita yaliibua maeneo mbalimbali ikiwamo kuongezeka kwa idadi ya watu na muda wa kuishi na hivyo kuongeza uhitaji wa huduma za afya.

"Kukua na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kutaongeza idadi ya watu wanaoishi mijini kufikia asilimia 50 kwa kipindi cha miaka 10 ijayo na kuongeza mahitaji ya huduma mbalimbali ikiwamo zinazosababisha ajali za barabarani," alisema.

# Wadau wa habari wamlilia Mkinga

Na Salome Kitomari

WAANDISHI wa habari nchini wamemlilia aliyekuwa mmoja wa wakurugenzi wa Kampuni ya Jamhuri Media, Wilbroad Mkinga (39), aliyefariki dunia jana katika

Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI).

Wakizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, wanahabari hao ambao walifanyakazi na Mkinga kwa nyakati tofauti, walisema ameacha pengo kubwa kwenye tasnia ya habari hasa katika habari za uchunguzi.

Mwanahabari nguli na aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa The Guardian Limited, Richard Mgamba, alisema Mkinga alikuwa mwajibikaji na aliyejituma kazini na kamwe hakukubali kushindwa bila kujali vikwazo vilivyopo.

"Alikuwa na vyanzo vingi vya habari, alijuana na watu wengi sana na alikuwa na namna yake ya kupata taarifa ambazo wengine hawakuziona. Ukimtuma kazi anakuletea vitu vya msingi, akiamini umemtuma kwa nia njema.

"Ameacha alama kwenye taaluma, waandishi wa habari wajifunze kuandika habari za kina na siyo kuimba mapambio. Mkinga alileta habari za tofauti ambazo wengine hawakuleta.

"Mfano siku moja nilikuwa kazini siku ya Jumapili, aliacha mapumziko, alikuja kunieleza kuwa kuna habari fulani na tulivyofuatilia ilikuwa kubwa na hakuna chombo kingine kilikuwa nayo," alisema.

Mgamba alisema waandishi wa habari wanapaswa kujikubali na kuipenda kazi yao kwa kuifanya kuwa ndiyo maisha na siyo kusubiri uteuzi au vyeo na kama vitatokea viwakukute wanafanya kazi yao kwa umahiri na weledi mkubwa.

"Wajikubali, wajithamini na kuwa wao pekee na kazi yao ina thamani sana, wasijione wanyonge. Mkinga angejiona mnyonge asingefika hapo alipofika. Hata ukikataliwa, hata ukitengwa pambana," alisema Mgamba ambaye aliwahi kushinda tuzo ya kimataifa ya CNN.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mwananchi, Bakari Machumu, alisema alifahamiana na Mkinga kati ya mwaka 2004 na 2006 ana atamkumbuka kwa uwezo mkubwa na vyanzo vingi vya habari.

"Alibobea kwenye habari za uchunguzi na habari mojawapo aliibua ya vyeti feki, alifanikiwa kupata cheti halisi cha kidato cha nne kwa njia za udanganyifu ili kuionyesha serikali kuna shida, habari ambayo ilisaidia serikali kuchukua hatua. Alikuwa mpambanaji mzuri mwenye kiu ya maendeleo kwenye tasnia," alisema Machumu.

"Ukizungumzia tasnia na habari za uchunguzi, alikuwa na sifa za peke, habari zake zilipaisha gazeti la The Citizen na waliachana naye baadaye kuingia kwenye siasa ambayo ni kinyume cha sera za kampuni," alisema.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Absalom Kibanda, alisema umahiri wa Mkinga ulidhihirika kutokana na kujizolea tuzo za umahiri kwenye uandishi wa habari ikiwamo mshindi wa jumla kutokana na kuandika habari za uchunguzi.

"Alikuwa mmoja wa watu wenye uwezo wa kujenga ushawishi kwa viongozi wa kisiasa na kiserikali, uhusiano wake haukuwahi kuvuruga au kuingiliana na uhusiano wake wa kikazi na kitaaluma, wanahabari na wahariri wenzake.

"Tulifahamiana kifamilia na kutofautiana mitazamo lakini tuliendelea kuwa marafiki," alisema Kibanda ambaye aliwahi kuwa Mhariri Mtendaji wa magazeti ya Tanzania Daima na Mtanzania.

Mhariri Mtendaji wa U-TV ya Azam TV, Frank Sanga, ambaye alifanya kazi na Mkinga wa Kampuni ya Mwananchi, alisema alikuwa mtu mwema, asiyekubali kushindwa na aliandika stori nyingi kubwa kwenye gazeti la The Citizen.

"Stori kubwa zilizoibua mjadala bungeni, ni mtu ambaye haogopi, akiamua kufanya kazi lazima atekeleze, alipenda mahojiano ya habari kubwa za uchunguzi, alipenda uandishi wa ukweli na siyo kubabaisha, tumepoteza miongoni mwa vijana ambao walihitajika sana kuitumia tasnia," alisema.

Meneja Mawasiliano wa UNICEF, Usiah Nkhoma, alisema alimpokea Mwananchi na kufanya naye kazi na kumfundisha kazi na tangu mwanzo alionyesha bidii na maono na ndoto ya kufika mbali kwenye tasnia.

Mwandishi nguli, Lucas Liganga, ambaye walishinda tuzo ya jumla kwa pamoja ya umahiri wa uandishi wa habari, alisema taifa limepoteza shujaa wa habari za uchunguzi ambaye alifanya habari hadi mwisho na alitafuta nyaraka zote muhimu bila kuchoka na mwenye utajiri wa vyanzo.

Mkurugenzi mwenza wa Jamhuri Media, Jacton Manyerere, alisema Mkinga alijisikia vibaya siku ya Jumamosi, akapelekwa Hospitali ya Kitengule na baadaye MOI ambako alifanyiwa upasuaji na kufariki jana alfajiri.

"Alikuwa mmoja wa wakurugenzi watatu akisimamia biashara, tunajadiliana na familia ila mazishi yatafanyika wiki ijayo kijijini kwao Chato," alisema.

# Lissu atua Kenya kwa kazi maalum

Na Mwandishi Wetu

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo Tanzania (CHADEMA), Tundu Lissu, jana aliwasili nchini Kenya kwa ajili ya uzinduzi wa kitabu chake.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Wakili wa Lissu, Prof. George Wajackoya, alisema kiongozi huyo aliwasili kwa ajili ya uzinduzi wa kitabu cha 'Kubaki katika Kivuli - Bunge na Uwajibikaji Afrika Mashariki (Remaining in the Shadows – Parlimanet and Accountability in East Africa).

"Lissu aliwasili hapa Nairobi na kesho (leo) tutakuwa kwenye uzinduzi wa kitabu na mambo yote mtayajua wakati wa uzinduzi," alisema.

Aidha, alisema kitabu hicho kinaeleza jinsi mabunge ya Afrika yalivyabaki kivuli baada ya ukoloni na kwamba kitasambazwa duniani kote.

"Kitasambazwa ulimwengu mzima, kitauzwa mtandaoni na kila mahali, tusubiri kesho tutajua maudhui mengi ya kitabu hicho," alisema Prof. Wajackoya.

Kuhusu uwezekano wa Lissu kurudi Tanzania baada ya kumaliza shughuli hiyo, alisema: "Siwezi kumruhusu kuja Tanzania ila akitaka kuja kwa hiari yake anaweza, ila kesho (leo) tutamsikia mwenyewe kama anakuja au la."

Lissu ambaye alikuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, alipigwa risasi 32 na watu wasiojulikana mwaka 2017 jijini Dodoma wakati akiendelea na majukumu yake ya kibunge.

Lissu ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alirejea nchini kwa mara ya kwanza mwaka jana na kugombea urais kwa tiketi ya CHADEMA na baadaya matokeo kutangazwa, alirejea Ubelgiji.

Kutokana na madhara ya risasi hizo, wiki tatu zilizopita alifanyiwa upasuaji wa 25 nchini humo, baadaye kutanguliwa na zingine zilizofanyika Kenya na Ubelgiji.






KUELEKEA SIKU 100 ZA RAIS SAMIA IKULU

# RAIS SAMIA ALIPOTUA RASMI MAPUTO KIKAO CHA SADC INAYOTIMIZA MIAKA 40

## ●Mwenyekiti afurahia mwanachama mama
## ●Mada; corona, tabianchi, ugaidi, uchumi

**Na Mary Geofrey**

LEO ni siku ya 98 tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipokula kiapo cha kuongoza taifa la Tanzania, Machi 19, mwaka huu.

Juzi akibakisha siku moja kutimiza wiki ya 14 madarakani, alikuwa jijini Maputo Msumbiji, akitumia siku hiyo kuhudhuria kikao cha dharura cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC),

Hapo mwenyeji wake, Mwenyekiti Rais Filipe Nyusi, wa Msumbiji alimpongeza Rais Samia kuwa mwanachama wa SADC kama Rais wa Tanzania na kwamba wanajivunia kuwa na mwanachama mwanamke.

Mkutano huo ulifanyika sambamba na maadhimisho ya miaka 40 tangu kuanzishwa SADC, ukiwa na kaulimbiu: "Kuimarisha amani na usalama, kuhamasisha maendeleo na ustahamilivu wa changamoto zinazoikabili dunia."

Kimsingi, Rais Samia si mgeni katika mikutano ya kimataifa akiwa katika hadhi ya wadhifa wa aina hiyo, bali ni mwendelezo wa majukumu yake tangu alipokuwa Makamu wa Rais kwa zaidi ya miaka mitano, alipomwakilisha mtangulizi wake, Hayati Rais Dk. John Magufuli.

Bado Rais Samia anabaki katika historia ya nyumbani na kimataifa, siku zote za ukuu wa nchi ameongoza Taifa katika nafasi ya mwanamke, ikibeba historia ya kipekee tangu uhuru wa nchi mwaka 1961 na tayari ameshafanya mengi kuimarisha umoja na misingi ya uwajibikaji kitaifa.




Rais Samia Suluhu Hassan akiondoka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Maputo, nchini Msumbiji juzi, baada ya kushiriki Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). **PICHA: IKULU**

Mnamo Aprili 22, mwaka huu, alihutubia kwa mara ya kwanza Bunge la Tanzania na akaahidi serikali yake itasimamia kwa umakini uhusiano baina ya Tanzania na nchi jirani na kuwa chachu ya kujenga jamii bora baina ya mataifa hayo.

Rais Samia aliainisha haja ya kuwaweka karibu majirani kwa vitendo na hadi sasa, mbali na Maputo, ameshafanya ziara tatu kwa kukutana kikazi na marais Uhuru Kenyatta, jijini Nairobi, Kenya na mara mbili kwa Yoweri Museveni.

Wakati ya kwanza nchini Uganda ilihusu uhusiano mwema, ya pili ni ilikuwa ya kutia saini mkataba unaohusu Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka nchini Uganda, wenye urefu wa kilomita 1,443 kutoka Magharibi mwa Uganda mpaka Bandari ya Tanga.

Mwanzoni mwa mwezi uliopita jijini Nairobi, alipata fursa ya kujadili uhusiano na Rais Kenyatta na kuingia baadhi ya makubaliano ya biashara, kuzuru bungeni na akahutubia umma kupitia wenyeji wake, Jukwaa la Wafanyabiashara.

**MKUTANONI SADC**

Juzi alikuwa katika kikao cha SADC, ambayo hadi hivi karibuni, Waziri wa Mambo ya Nje na Uhusiano Kimataifa, Dk. Stergomena Tax, alikuwa Katibu Mtendaji wake na Hayati Dk. Magufuli, ndiye alimpa kijiti Rais Nyusi, mwenye historia pia ya kuishi Tanzania.

Akiwa katika mkutano huo, Rais Samia, alitambulishwa na mwenyeji Rais Nyusi, ambako walijadili ajenda zinazohusu mtangamano wa nchi wanachama wa jumuiya hiyo, fursa zao kiuchumi na changamoto za usalama.

**SADC NA UGAIDI**

Mwenyekiti Rais Nyusi, anasema jitihada za pamoja kutoka nchi wanachama wa ukanda wa SADC zinahitajika zaidi katika kukabiliana na tatizo la ugaidi linaloikabili nchi hiyo, kwa sababu limekuwa likirudisha nyuma juhudi za maendeleo kwa nchi wanachama.

"Mifumo yetu itumike kutambua kuwa ugaidi ni tishio la kimataifa, ili kuweza kupambana nao tunatakiwa kuwa na ufahamu wa kina kuhusu ugaidi, tuweze kuuondoa katika eneo letu lote," anasisitiza.

Rais Nyusi anaendelea: "Napenda kuwaeleza kuwa hapa kwetu Msumbiji tunatambua vyema wajibu wetu, mshikamano, msaada tunaopata kutoka SADC na nchi marafiki wanaosaidia jitihada zetu ili kuhakikisha ugaidi unaondoka."

Anasisitiza kwamba wanatambua msaada kubwa kutoka SADC katika kuwaletea amani na mshikamano kitaifa.

**HATIMA IJAYO**

Mengine yaliyokuwa ajenda muhimu na kujadiliwa, ni mlipuko wa janga la ugonjwa wa Covid-19 na namna maambukizi yake na virusi yanavyokabiliwa.

Mwenyekiti Rais Nyusi, anasisitiza nchi wanachama ziendelee kuunga mkono jitihada za taasisi za utafiti katika kufuatilia taarifa za kusambaa maradhi ya Covid-19 na mawimbi yake mapya ya kusambaa, pia namna ya kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi mapya.

"Virusi hivi ni jambo ambalo hakuna nchi inaweza kupambana yenyewe bila ya kushirikiana na nchi nyingine," anasisitiza Rais Nyusi.

Ana rai ya kuzisihi nchi wanachama kushirikiana kusambaza taarifa katika lugha zilizo sahihi na kuendelea kuwaelimisha wananchi kutimiza majukumu yao kujikinga.

Hapo, anajenga hoja ya kuanzishwa kituo cha majanga, masuala ya mabadiliko ya tabianchi, usalama wa chakula, biashara na uwekezaji katika ukanda wa SADC.

Kuhusu jukwaa la kukuza uchumi, anasema wameshakutana na Jukwaa la Sekta Binafsi katika kuwekeza katika sekta ya biashara katika jumuiya hiyo ili kuleta mageuzi ya kiuchumi ya mataifa yao.

"Jukwaa hili ni la kusambaza taarifa mbalimbali zilizopo katika sekta ya kilimo na kuwa na mahusiano mapya na mataifa mengi na kukuza dhamira ya kuleta maendeleo," anasema Nyusi. Katika hali ya tabianchi, Rais Nyusi anasema baadhi ya nchi wanachama zimekumbwa na uhaba wa mvua na nyingine zina mvua nyingi zaidi, hata kusababisha uwezekano kwa baadhi ya nchi kukumbwa na uhaba wa chakula.

Anasema nchi hizo zinapaswa kuwa na jitihada na kufikia malengo ya jumuiya hiyo kwa maendeleo ya wananchi wao.

Mkutano huo umefanyika sambamba na maadhimisho ya miaka 40 tangu kuanzishwa SADC ikiwa na kauli mbiu "kuimarisha amani na usalama, kuhamasisha maendeleo na ustahamilivu wa changamoto zinazoikabili dunia."

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 57 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**SEBALDA CHARLES LESHABARI**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**MELKIZEDECK THOMAS LELSHABARI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanini ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 5th Mwezi wa July, 2021.

**Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 10th Mwezi June, 2021.**

NAIBU MSAJILI

216328202

HABARI KITAIFA

# Mabadiliko sera, sheria kutomwacha nyuma mwanafunzi aliyepata ujauzito

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema inatarajia kupitia sheria ya elimu, sera na mitaala ili kuhakikisha pamoja na mambo mengine mwanafunzi mjamzito haachwi nyuma katika elimu.

Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa kongamano la siku moja la wadau na wachangiaji wa mfuko wa elimu lililoandaliwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Kongamano hilo ambalo liliwakutanisha wadau lilipata fursa kwao kuona miradi mbalimbali iliyotekelezwa na TEA kwa kipindi cha miaka mitano kilichoanzia mwaka 2015 na itakayotekelezwa kwa mwaka wa fedha ujao.

Akijibu swali la mwandishi wa habari kuhusu lililotaka mkakati wa serikali kuhakikisha mwanafunzi wa kike aliyepata ujauzito haachwi nyuma kielimu, Kipanga alisema wanakwenda kupitia upya sera, sheria na mitaala ya elimu.

"Mkakati huu upo na kwa vile tunakwenda kupitia upya sera ya elimu, sheria ya elimu na mitaala mambo haya yote msiwe na wasiwasi yanakwenda kuwekwa sawa.

"Si kwamba haikuwapo, ilikuwapo hata wakipata ujauzito kuna njia mbadala walikuwa wanatumia kutatua. Hili nalo tutakwenda kulijadili ili kuzingatia namna gani vijana wetu wanapata elimu ili mradi kila Mtanzania mwenye fursa ya kupata elimu, kuhakikisha anaipata na hakuna atakayeachwa nyuma kwa sababu yoyote ile," alisema.

Kuhusu kongamano hilo, Kipanga alisema kupitia TEA ambayo ipo ndani ya wizara hiyo wameona inafaa kushirikisha wadau wa maendeleo kuona namna gani wanaweza kushiriki katika eneo la miundombinu wakati serikali ikisimamia sera.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye, alisema jukumu la msingi la mfuko wa elimu wa taifa unaoratibiwa na mamlaka hiyo ni kuongeza jitihada za serikali katika kuboresha miundombinu ya elimu ili kuwa na ubora.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2019/20, zaidi ya Sh. bilioni 9.1 zilitumika kufadhili miradi 96 ya elimu katika shule 88 na taasisi moja ya sayansi na teknolojia.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya shule 116 zimenufaika na miradi 123 inayogharimu jumla ya Sh. bilioni 9.4.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano kilichoanzia mwaka 2015 takribani Sh. bilioni 92 zilitolewa mfuko wa elimu kwa ajili ya kufadhili utekelezaji wa miradi mbalimbali ya elimu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu 254 katika shule za msingi na sekondari.

"Ujenzi wa mabweni 54, ujenzi wa nyumba 450, vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo takribani 1,680, tulishiriki katika ukarabati wa shule kongwe 17 ambao ulikuwa ni mradi wa ukarabati wa shule kongwe 89 uliokuwa unaratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Pia alisema wamenunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia na ujenzi wa miundombinu katika shule 33 kwenye shule zenye wanafunzi wenye uhitaji maalum.

Meneja Miradi wa TEA, Masozi Nyirenda, alitaja miradi ambayo wameitekeleza kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 na 2020/21 ni pamoja na ukarabati shule kongwe za sekondari 17 katika eneo la madarasa, ofisi, bwalo la chakula na maabara.

Pia alisema wamefanya ujenzi wa miundombinu ya elimu katika shule za msingi na sekondari na shule mbili za wenye ulemavu kwa kuwajengea madarasa.



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya Maski and Sons Ltd, wakiendelea na ujenzi wa daraja katika eneo la Kitunda, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: NASRA HUSSEIN/ TUDARCO**

# Kunyimwa unyumba chanzo utitiri talaka

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya wanaume wa Kata ya Wendele, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wamelalamikia kitendo cha kunyimwa unyumba na wake zao, wakibainisha kuwa ni kiini cha ndoa nyingi kuvunjika, kutelekeza watoto na kuoa wanawake wengine.

Walitoa malalamiko hayo juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia kwa Wazee yaliyofanyika kiwilaya katika Kijiji cha Wendele chini ya Baraza la Wazee la Halmashauri hiyo.

Mmoja wa wanaume hao, Joseph Kandi (45), alisema tatizo la wanaume kunyimwa unyumba na wake zao limekuwa kubwa kwenye jamii na wanaume wengi wanaogopa kwenda kwenye mdawati ya jinsia kupata msaada kwa kuona aibu na kuamua kuvunja ndoa.

"Wanaume tunanyimwa unyumba na wake zetu na tukijaribu kuwahoji wanatishia kuvunja ndoa. Tunaomba serikali hasa kitengo cha dawati la jinsia na ustawi wa jamii iingilie kati suala hili. Watoto wanakosa malezi ya baba na mama," alilalamika Kandi.

Dalali Musa, mkazi mwingine wa kijiji hicho, alisema suala hilo linapaswa kushughulikiwa kwa haraka, akitahadharisha kuwa lisipopatiwa ufumbuzi, linaweza kusababisha kuwapo kwa migogoro isiyokuwa na tija na ongezeko kubwa la watoto wa mitaani.

Alisema ndoa zinapovunjika wanaopata shida ni watoto wadogo na kwamba si tu wanawake na watoto wanafanyiwa vitendo vya kikatili, bali wanaume ni waathirika wakubwa wa vitendo hivyo ila wanaona aibu kwenda kushtaki kwenye vyombo vya dola.

Mkuu wa Dawati la Jinsia, Kituo cha Polisi Kahama, Tiho Masatu, alisema wanaume wengi wamekuwa wakifanyiwa ukatili wa kimwili na kihisia na wenzi wao kwa kunyimwa unyumba na kukosa sehemu ya kuelezea kero zao, hali ambayo imesababisha kuvunjika kwa ndoa nyingi.

Hata hivyo, aliwataka wanaume kwenda kwenye vituo vya polisi na kuwasilisha malalamiko yao kwa dawati la jinsia kama ambavyo wamekuwa wakifanya kinamama na watoto wadogo wanaofanyiwa ukatili wa kinjisia, ili kupata suluhu ya migogoro ya ndoa zao kabla ya kuchukua uamuzi wa kutengana.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Jonathan Shayo, ambaye ni mratibu wa masuala ya wazee, alisema migogoro ya wanandoa na kuvunjika kwa ndoa inasababisha ongezeko la ukatili dhidi ya watoto wanaokosa haki za malezi ya wazazi.

Aliwataka wanaume kuvunja ukimya kwa kueleza kero zao kwenye vyombo vya sheria likiwamo dawati la jinsia na ustawi wa jamii ili kuangalia namna ya kutatua kero hizo kuliko kuchukua uamuzi wa kuvunja ndoa na kuoa wanawake wengine.

Hivi karibuni, serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, ilibainisha kuwapo kasi ya ongezeko la talaka nchini, ikiwataka viongozi wa dini kulimulika suala hilo lenye madhara makubwa kwa ustawi wa watoto na jamii kwa ujumla.


## EMPLOYMENT OPPORTUNITY

**A LEADING SISAL ESTATE IN TANGA REGION IS INVITING APPLICATIONS FROM QUALIFIED CANDIDATES FOR THE POSITION OF: ACCOUNTS MANAGER**

**JOB SCOPE**
To effectively and efficiently manage the Estate Finance, Accounts and function.

**JOB DESCRIPTION**
The role entails managing the following key aspects within the company:
- Maintain Financial Accounts
- Ensure all Statutory Compliances
- Prepare Financial / MIS Reports
- Financial Planning and Budgeting
- Efficient Funds Management
- Maintain Banking Relationships
- Exercise Internal Control and Audits
- Support Exports and Commercial functions

**POSITION REQUIREMENTS**
**EDUCATION:** Qualifications; CPA or ACA or ACCA or equivalent

**PROFESSIONAL EXPERIENCE AND REQUIREMENTS:**
- 5-7 Years in a similar function or role
- Preference to candidates who have worked in similar Plantation or Estates

**LOCATION**
The position is based on the estate in Lugongo -Tanga Region and reports to the General Manager

**SALARY AND BENEFITS**
Shall be commensurate with the candidates experience and position

**TO APPLY:**
If you are confident that you match the above-mentioned criteria, please send your C.V within 7 days to the following email address mentioning the position in the subject line to:
**operations@mactz.co.tz**

21632720I

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi wanataka uwajibikaji wenye tija

**HIVI** karibuni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, alieleza jumla ya watumishi wa umma 70,437 kati ya 91,841 wamepandishwa madaraja na tayari zimetolewa Sh. bilioni 300 za kuwalipa.

Aidha, Sh. bilioni 23 zimetolewa kulipa malimbikizo kwa watumishi 11,983 ikiwamo walimu.

Hii ni habari njema kwa watumishi ambao kwa muda mrefu walisubiri kupandishwa madaraja na kulipwa stahiki zao mbalimbali kwa mujibu wa sheria.

Tunaipongeza serikali kwa hatua hii, tunaamini morali ya kazi itaongezeka kwa kuwa kilio cha muda mrefu cha watumishi ni kulipwa stahiki zao muhimu kwa wakati, kiasi cha wengi kusota kwa muda mrefu katika daraja moja la kazi, na kila maadhimisho ya siku ya wafanyakazi Mei Mosi, walipaza sauti zao kuhusu jambo hilo.

Rais Samia Suluhu Hassan amesikia kilio chao na sasa ametekeleza, jambo ambalo ni deni kwa watumishi kufanyakazi kwa bidii ili kuleta matokeo chanya kwa Watanzania.

Katika hotuba zake zote Rais Samia amesisitiza uwajibikaji wa watumishi wa umma, ili kuhakikisha miradi na shughuli za serikali za kuwahudumia wananchi zinakamilika kikamilifu na kwa wakati.

Ipo miradi mingi ya maendeleo ambayo inagusa maisha ya wananchi moja kwa moja, inahitaji usimamizi wa karibu na umakini wa watumishi wa umma ili kufikia lengo.

Miongoni mwao wapo watumishi wa sekta za afya ambao wana wajibu wa kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali mbalimbali nchini, ikiwamo kuhakikisha hakuna wizi wa dawa na vifaa tiba vingine muhimu.

Pia, kwa walimu wanawajibu wa kufundisha kwa bidii ili kuongeza kiwango cha ufaulu na uelewa wa masomo kwa wanafunzi na kuwa na taifa bora la sasa na baadaye.

Watumishi wa umma watambue kuwa fedha wanayolipwa inatokana na kodi za Watanzania ambao wao wanapaswa kuwalipa kwa utumishi uliotukuka ambao unalengo la kutatua kero za wananchi wa kawaida.

Kiasi cha fedha kilichotolewa na serikali ni kikubwa na sasa tunataka kuona uwajibikaji wenye tija na kuondokana na kufanyakazi kwa mazoea.

Wapo wanaosema kuwa uwajibikaji na kufanyakazi kwa bidii kupo sekta binafsi kutokana na ufuatiliaji wa karibu na ajira za mkataba hivyo mwajiriwa anapaswa kufanyakazi kwa bidii ili aongezewe mkataba na aendelee kuwapo kazini.

Wengi wanaamini wakishaingia serikalini ni ajira ya kudumu hadi atakapostaafu na wengi hufanyakazi watakavyo kwa maana ya kuzingatia muda wa kuingia na kutoka, lakini utendaji kazi bado siyo wenye tija.

Tunatarajia kuimarisha kwa mifumo ya ufuatiliaji utendaji kazi wa watumishi wa umma ili tija ya kodi ya Mtanzania ionekane kupitia kazi ambazo zitaleta matunda katika maisha ya wananchi.

Ikiwa kutakuwa na uwajibikaji hatutaona mabango, malalamiko mara viongozi wa kitaifa wanapofika kwenye maeneo yao kwa kuwa mambo mengi yatakuwa yametatuliwa.

Kama serikali inatimiza wajibu wake basi watumishi wahesabu ni deni kwao sasa ni wakati wa kuwajibika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wabunge sio kwenu tu 'vyuma vimekaza' kote

**KABLA** ya kuendelea, nianze kwa kupongeza uamuzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa kumweka sawa mbunge wake anayeomba nyongeza ya posho na mshahara na kumtaka ahudumie wananchi kwa kufuata utaratibu wa nchi.

Zaidi ya hapo, chama chake kinamtaka mbunge ahamie nchi nyingine ambayo wabunge wanalipwa kwa pesa dola za |Kimarekani, kama ambavyo anataka Bunge la Jamhuri ya Tanzania, nalo lifanye hivyo kwa wabunge wake.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, amwelekeza mbunge huyo kuhudumia wananchi wa jimbo lake, au kuchagua kuhamia katika nchi ambazo zinalipa wabunge wake kwa dola.

Chama chake kimeamua kumweka sawa, kutokana na mbunge huyo kuchangia mjadala wa makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha na kuomba serikali iangalie upya maslahi ya wabunge. Akatoa mfano wa mabunge ya Afrika Kusini na Kenya, kwamba wabunge wake wamekuwa wakilipwa mishahara na posho nzuri, huku akidai kwamba maslahi ya wabunge wa Tanzania hayatoshelezi.

Pamoja na hayo kuna umuhimu wa kumkumbusha mbunge huyo, kuwa fedha za walipa kodi zina majukumu mengi ya muhimu, hivyo kuangalia upande wake tu na kusahau kwingine si vizuri.

Ikumbukwe kuwa, hata Rais Samia Suluhu Hassan, hakuongeza mishahara kwenye kilele cha Siku ya Wafanyakazi Duniani, kwa kuwa hali si nzuri na akawa ameahidi kufanya hivyo mwaka ujao.

Hivyo, si vibaya kuvumilia na hasa kwa kuzingatia wapo watumishi wengi tu katika sekta za umma wakiwamo walimu wamekuwa wakidai malikimbikizo yao, kwa muda mrefu, wanahitaji kusemewa huko bungeni.

Nimetoa mfano mdogo wa walimu tu, lakini ninaamini yapo maeneo mengi ambayo yanategemea hizo fedha iwe ni kwa ajili ya mishahara au shughuli nyingine za maendeleo ya nchi hii.

Pia inawezekana jimboni mwake kuna kero nyingi zinazotakiwa kuwasilishwa bungeni, ili zipatiwe ufumbuzi, badala yake analilia kuongezwa posho na mshahara.

Ni vyema kama mzalendo na mwakilishi wa kweli, wakaanza na kutetea pia maslahi ya watumishi wa sekta nyingine za umma, ambako hawana hiyo posho ya kutwa kama ambayo wabunge wanapata.

Ajiulize, inakuwaje kwa wapigakura wake ambao baadhi hawajui hata mlo wa siku ni shida, hali kadhalika kuna wanaolipwa uwe mtumishi wa umma au binafsi, hata kujiajiri, posho ya mheshimiwa kwa siku tatu au nne, ni sawa na malipo ya mwezi ya mpigakura huyo. Je, hiyo imekaa vipi?

Ni bahati nzuri kwamba, ubunge wa jimbo, mtu anaomba mwenyewe kuwakilisha wananchi, hivyo aliyeona posho na mshahara havitoshi, anaweza kuachia ngazi wananchi wakachagua mwakilishi mwingine.

Miaka kadhaa iliyopita, gazeti hili lilichapisha taarifa kuhusu stahiki za wabunge nchini, zikiwamo posho za vikao Sh. 220,000 kwa siku, za chakula na malazi 120,000 kwa siku, zinazolipwa wakiwa kwenye shughuli za bunge.

Mbali na posho hizo, wabunge pia wanalipwa mshahara wa mamilioni, huku wakipata zaidi ya Sh. milioni 200 zisizokatwa kodi, kwa ajili ya kiinua mgongo wanapomaliza miaka mitano ya kila bunge.

Itoshe kusema kuwa huyo mbunge anayeomba kuongezwa posho na mshahara, Mungu anamuona, hivyo ni vyema akaangalie maslahi mapana ya jimbo lake na taifa kwa ujumla badala ya kuangalia ubunge tu.

Kimsingi, wananchi wote hawawezi kwenda bungeni, badala yake wanachagua wawakilishi wa kuwasemea kero za maeneo yao na siyo kwenda kutafuta posho na mishahara mikubwa.

Vilevile, mbunge si mfadhili wa wananchi kwamba aka-ongezewe posho na mshahara ili akawagawie, bali anakwenda bungeni kuweka msukumo ili kero za jimbo lake zitafutiwe ufumbuzi.

Yeye kutaka wananchi waambiwe kuwa bungeni hakuna kitu, kwamba wabunge wamekuwa wakitukanwa mitandaoni kuwa wanalipwa pesa nyingi, inaonyesha kuwa kazi hiyo ni ya kufadhili wapiga kura.

Msisitizo wake katika kujenga hoja ya kutaka maslahi zaidi, anasema, pesa ya posho inayolipwa bungeni haitoshi, mishahara haitoshi, hivyo atasema ukweli daima, kwa madai kwamba fitina kwake ni mwiko.

Inawezekana hilo likawa na ukweli ndani yake, lakini ni muhimu pia kuangalia na maeneo mengine, kwani nayo yanategemea fedha hizo hizo za walipa kodi, ili kila upande unufaike na kile kidogo kinachopatikana.

# Wafutiwa kesi utakatishaji fedha

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imefuta shtaka la kutakatisha fedha lililokuwa linawakabili washtakiwa saba waliodaiwa kujipatia Sh. bilioni 4.7 kwa njia ya udanganyifu kutoka Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Washtakiwa ni Baraka Madafu, Lusekelo Mbwele, Leena Joseph, Mark Mposo, Benard Mndolwa na Silvina Karugaba ambao wanatuhumiwa kwa mashtaka 10 yakiwamo manne ya kughushi, manne ya kuwasilisha nyaraka za uongo, kujihusisha na genge la uhalifu na kujipatia Sh. bilioni 4.78 kwa udanganyifu.

Washtakiwa hao walifutiwa mashtaka yao jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Kassian Matembele, baada ya Jamhuri kuomba kufanya hivyo.

Akiiwakilisha Jamhuri, Wakili wa Serikali, Faraja Nguka, alidai shauri lilikuja kwa ajili ya kutajwa na kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa niaba ya Jamhuri, hana nia ya kuendelea kuwashtaki washtakiwa wote saba kwa shtaka la 11 la kutakatisha fedha.

Nguka alidai Jamhuri haina nia ya kuwashtaki kwa kosa hilo, hivyo chini ya kifungu cha 234(1) cha Sheria ya Makosa ya Jinai anaomba kuwasomea washtakiwa hati mpya ya mashtaka.

Mahakama iliwafutia shtaka hilo la kutakatisha fedha washtakiwa wote na kuruhusu upande wa mashtaka kusoma hati mpya ya mashtaka.

Akisoma hati hiyo, Wakili Nguka alidai washtakiwa wanakabiliwa na jumla ya mashtaka 10, yakiwamo ya kughushi mkataba wa udhamini na barua ya Bodi ya Wadhamini wakionyesha kwamba bodi inawatambulisha watumishi kuwa ni wafanyakazi wa kudumu wa Kampuni ya Peertech.

Washtakiwa wanadaiwa kudanganya kwamba wafanyakazi 78 wa Kampuni ya Peertech ni wafanyakazi wa kudumu na kampuni hiyo na imewadhamini wapewe mkopo wa Sh. 4,786,800,000 na Benki ya NBC wakati ni uongo.

Inadaiwa kati ya Desemba 4 mwaka 2018 na Desemba 3 mwaka 2020, katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam, washatakiwa hao walijihusisha na genge la uhalifu na kujipatia Sh. bilioni 4.787 kwa udanganyifu.

Katika shtaka la pili, inadaiwa katika kipindi hicho, washtakiwa walighushi mkataba wa udhamini wa mkopo wakionyesha watumishi 60 ni waajiriwa wa Kampuni ya Peertech na wana mikataba ya kudumu, hivyo kampuni inawadhamini kupata mkopo. Katika shtaka la tatu, wanadaiwa kuwasilisha nyaraka hizo NBC Masaki huku wakijua zimeghushiwa.

Inadaiwa katika shtaka la nne washtakiwa walighushi taarifa ya Bodi ya Wadhamini ikiwatambulisha wafanyakazi 11, wakawasilisha nyaraka hizo benki, kisha wakaghushi tena kwa wafanyakazi 20, wakawasilisha benki na kuwasilisha nyaraka za uongo Benki ya NBC.

Katika shtaka la 10, washtakiwa wote wanadaiwa kujipatia zaidi ya Sh. bilioni nne kati ya Desemba 4 mwaka 2018 na Desemba 31 mwaka 2020 katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam kwa kutoa nyaraka za uongo NBC Masaki wakionyesha kwamba wafanyakazi 78 waajiriwa wenye mikataba ya kudumu na Kampuni ya Peertech imewadhamini kupata mikopo.

Hakimu Matembele aliwafahamisha washtakiwa kwamba mashtaka yanayowakabili ni ya uhujumu uchumi, hivyo dhamana wanatakiwa kuomba Mahakama Kuu.

Baada ya kusema hayo, mahakama iliahirisha kesi hadi Julai 6 mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

## Wapatiwa mafunzo ya kuandika wosia

**Na Mwandishi Wetu,** KAGERA

MILA potofu na kukosekana kwa uadilifu katika jamii kumechangia kuongezeka kwa matukio ya kunyang'anywa mali, kunyanyaswa, kuteswa kwa wajane na kuwasababisha watoto walioachwa na marehemu kukosa malezi sahihi na hatimaye kuishia mitaani na kuwa ombaomba.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge, alisema hayo wakati wa mafunzo maalum yaliyoendana na maadhimisho ya Siku ya Wajane Duniani kwa lengo la kuwajengea uwezo Makatibu Tawala wa wilaya na Maofisa Tarafa wa mikoa ya Kigoma na Kagera kuhusu kuandika na kuhifadhi wosia, usimamizi wa mirathi pamoja na huduma nyingine zinazotolewa na RITA.

Katibu Tawala wa mkoa huo, Prof. Faustin Kamuzora, akiwasilisha hotuba ya maadhishimisho hayo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, amewaagiza viongozi kupitia ngazi zote kutafuta ufumbuzi wa haraka kuhusu kuongezeka kwa migogoro ya mirathi inayosababishwa kwa makusudi na baadhi ya wanandugu kwa makusudi.

Pia aliwaagiza viongozi wa mkoa kuanzia vitongoji, vijiji, kata na wilaya, kushughulikia na kumaliza migogoro ya mirathi inayosababishwa na ndugu wa marehemu wenye nia mbaya na kukosa huruma na kuwasababishia wajane na watoto kuishi kwa kutangatanga kwa kukosa msaada wa huduma mbalimbali ikiwamo malazi, chakula, mavazi na watoto kuacha shule.

Mwakilishi wa wajane Mkoa wa Kagera, Winifrida Rwezaula, alisema kupitia risala yake kuwa wajane wengi wanakosa ushirikiano mzuri kutoka katika vyombo mbalimbali vya uamuzi kutokana na kundi hilo kutokutiliwa mkazo stahiki.

Alitoa ombi kwa serikali kutambua rasmi kuwapo kwa wajane katika jamii ya Watanzania na kuandaa mikakati ya kuwahusisha katika kila ngazi ya uamuzi kuanzia serikali ya kijiji, mtaa hadi serikali kuu.

Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu, Emmy Hudson, alisema RITA ilianzisha huduma ya kuandika na kutunza wosia baada ya kuona mashauri ya mirathi yanaongezeka kwa kasi na kuchukua muda mrefu kukamilika na warithi kuchelewa kupata haki zao.

Alitoa wito kwa jamii kuacha kuogopa kuandika wosia kwa kuamini kwamba ni kujichulia.




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, akizungumza katika kongamano la Siku ya Walimu na NMB, jijini Dar es Salaam juzi. Lengo la kongamano hilo ni kuwapa mafunzo na elimu juu ya bidhaa za benki hiyo, zitakavyoweza kuwasaidia kwa maisha ya baadaye. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkapa akumbukwa kwa kuboresha afya

**Na Richard Makore,** MUSOMA

WADAU wa sekta ya afya Kanda ya Ziwa wamesema watamkumbuka Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa, kwa kusaidia sekta hiyo kupitia taasisi yake ya Benjamin Mkapa Foundation (BMF).

Walitoa maoni hayo jana katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma Vijijini mkoani Mara, ikiwa zimebaki siku chache kuadhimisha kumbukizi ya mwaka mmoja wa kifo chake. Mkapa alifariki dunia Julai, mwaka jana.

Akizungumza na Nipashe, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mara, Dk. Frolian Tinuga, alisema Mkapa alikuwa na maono katika kusaidia sekta ya afya ndiyo maana alianzisha BMF kwa lengo la kusaidia Watanzania.

BMF, alisema tangu kuanzishwa kwake, imesaidai upatikanaji wa watumishi 128 wa sekta ya afya mkoani Mara. Dk. Tinuga alisema licha ya kuwezesha upatikanaji wa watumishi, pia kuna wataalamu waliosomeshwa na BMF na kuajiriwa sekta binafsi na serikalini katika sekta ya afya nchini. Aliongeza kuwa Mkapa alitumia muda wake baada ya kustaafu kuhakikisha taasisi yake inajikita kusaidia jamii kupunguza uhaba wa watumishi na upatikanaji wa huduma bora za afya.

Naye Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Murangi, Dk. Yusuph Wambura, alisema maono ya hayati Mkapa yamesaidia kuboresha huduma za afya.

Alisema kabla ya kuwapo BMF, walikuwa na uhaba wa watumishi sekta ya afya hususani upande wa upasuaji lakini kwa sasa wanahudumia wanawake 150 hadi 160 wanaojifungua kwa mwezi na kwa siku wanahudumia wagonjwa wa nje kati ya 50 na 70 kwa siku.

Pia Dk. Wambura alisema kituo hicho kina uwezo wa kulaza wagonjwa 25 hadi 30 wanaotoka kata 16. Alisema alisema mpaka sasa wamesaidiwa watumishi zaidi ya 10 akiwamo daktari wa dawa za usingizi pamoja na wauguzi.

Akizungumzia huduma za afya, Mratibu wa BMF Kanda ya Ziwa, Dk. Remmy Moshi, alisema taasisi hiyo imekuwa msaada kwa kutoa watumishi katika zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Alisema BMF imewezesha upatikanaji wa watumishi 128 wa taaluma tofauti katika sekta ya afya.

Pia alisema BMF imekuwa na jukumu la kuziba nafasi mbalimbali ambazo kuna uhaba wa watumishi na kwamba jambo hilo limefanikiwa kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

# BoT yaonya watoa huduma za fedha

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI Kuu (BoT) imesema watoa huduma ndogo za fedha daraja la pili ambao walikuwa hawajajisajili kufikia Aprili 30 mwaka huu, hawataruhusiwa kutoa huduma hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Gavana wa BoT, Profesa Florens Luoga, tayari benki hiyo imetoa orodha ya watoa huduma ndogo za fedha wa daraja hilo 446 ambao wamejisajili.

Alisema watoa huduma ndogo za fedha wa daraja hilo ambao hawakuwasilisha maombi ya leseni kwenye benki hiyo, hawapaswi kuendelea kufanya biashara ya huduma hizo ndogo za fedha.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 57 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018, watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili ambao hawakuwa wamewasilisha maombi ya leseni Benki Kuu kabla ya Aprili 30 mwaka huu, hawapaswi kuendelea kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha hadi wawe wamepata leseni.

"Kuendelea kufanya biashara bila kuwa na leseni ya Benki Kuu ni uvunjifu wa sheria unaoweza kupelekea faini au kifungo kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018.

"Orodha hii inatolewa kwa mujibu wa kifungu cha 55(a) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018," alisema Profesa Luoga katika taarifa yake hiyo.

Alisema BoT itaendelea kutoa machapisho ya orodha iliyohuishwa ya watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili waliosajiliwa, ikiwamo orodha ya watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la tatu na la nne.

Katika orodha hiyo idadi ya watoa huduma kwa kila mkoa na idadi yao ni Dar es Salaam (129), Mwanza (45), Dodoma (28), Arusha (29), Morogoro (29), Mbeya (22), Pwani (16), Mara (17), Mtwara (14), Shinyanga (14), Iringa (13), Ruvuma (10), Kagera (9), Songwe (9), Tabora (9), Lindi (7), Singida (7), Manyara (7), Njombe (7), Kigoma (6), Tanga (6), Kilimanjaro (5), Geita (5), Simiyu (3) na Katavi (2).

Daraja la pili ni taasisi zinazotoa mikopo bila kupokea amana za umma ikujiumuisha kampuni za kukopesha watoa huduma ndogo kwa njia za kidijitali na watu binafsi wanaokopesha.

Kwa mujibu wa kanuni vigezo vya leseni ada ya Sh. 500,000 kwa kampuni au Sh. 300,000 kwa watu binafsi, kisha BoT itafanya tathmini ya uwezo wa kifedha, uzoefu, sifa na uadilifu wa wamiliki, wajumbe wa bodi na viongozi.

# Wajasiriamali kufaidika na akaunti ya 'Hodari'

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB jana imezindua akaunti ya wajasiriamali katika sekta mbalimbali nchini iliyopewa jina la 'Hodari' ili kuwasaidia kuboresha biashara zao.

Uzinduzi huo umeenda sambamba na uzinduzi wa msimu wa pili wa kampeni ya "Tupo Mtaani Kwako" inayolenga kuhamasisha matumizi ya huduma za benki na kuwapa Watanzania elimu ya fedha na uwekezaji.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika katika viwanja vya Mbagala Zakhiem, jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Bruce Mwile, alisema akaunti hiyo itarahisisha biashara za wajasiriamali kwa kuwawezesha kuweka akiba kwa urahisi, kupokea malipo kidijitali kupitia CRDB Lipa Namba na kuunganisha na fursa za uwezeshaji kupitia mikopo ya wajasiriamali.

Bruce alisema pamoja na kuboresha biashara za wajasiriamali, akaunti hiyo pia inatoa unafuu mkubwa kwa kuwa wateja hawatatozwa makato yoyote kwa miamala ambayo itafanyika ndani ya mtandao wa Benki ya CRDB kuanzia kwenye matawi, CRDB Wakala, ATMs na SimBanking. Pia, akaunti hiyo itafunguliwa bure ili kuwafikia wajasiriamali wengi zaidi hususani wale wenye mitaji midogo.

"Uzinduzi wa akaunti ya 'Hodari' unakuja wiki chache baada ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kuhimiza taasisi za fedha kuja na mikakati ya uwezeshaji kwa wajasiriamali ambao wengi wao ni vijana," alisema Bruce.

Aliwaomba kufungua akaunti hiyo kwa kuwa huduma hiyo ni kwa wajasiriamali wote iwe bodaboda, mama/ baba lishe, wauza genge, wenye maduka ya reja reja, wamachinga na wengine wote.

Uzinduzi wa akaunti hiyo ni mwendelezo wa utekelezaji wa maoni ambayo benki hiyo ilipokea kutoka kwa wateja wake katika msimu wa kwanza wa kampeni ya "Tupo Mtaani Kwako," mwaka jana.

"Katika kampeni ya mwaka jana vilevile tulipata mrejesho kuhusu bima, ambapo hivi karibuni benki yetu ilizindua kampeni maalumu ya elimu ya bima kwa umma yenye kaulimbiu ya "Furahia Maisha. Bima Unachokithamini, jitihada zote ni matokeo ya kufanyia kazi maoni ya wateja wetu na wananchi kwa ujumla," alisisitiza.

Katika kampeni ya "Tupo Mtaani Kwako" ya mwaka huu Benki ya CRDB imejipanga kutumia timu ya wafanyakazi wake wabobevu katika masuala ya kibenki kuwatembelea wateja popote pale walipo, iwe ni ofisini, sokoni, dukani, stendi na kuwapatia huduma.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Bruce Mwile (kulia), akiwa na Mkurugenzi wa wateja wa kati na wadogo wa benki hiyo, Boma Raballa, Meneja wa Benki hiyo Kanda ya Mashariki, Badru Idd na maofisa waandamizi, wakipeperusha bendera kuashiria uzinduzi wa kampeni ya 'Tupo mtaani kwako'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makandarasi wazawa wataka ushiriki miradi ya kimkakati

**Na Anaeli Mbise**

MAKANDARASI wazawa nchini wameeleza utayari wao wa kushiriki katika ujenzi wa miradi ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa nchini.

Akizungumza na Nipashe jana mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Building Work, Mhandisi Mohamed Noray, alisema kuwa makandarasi wa ndani wana uwezo na ujuzi wa kufanya miradi hiyo kukamilika vizuri.

"Nimefanya shughuli kadhaa za ujenzi katika sehemu tofauti za nchi na kupitishwa na bodi zinazohusika," alisema.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, endapo serikali itaendelea kumwamini atazidi kufanya kazi kwa weledi pamoja na kumaliza kwa wakati.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa zamani wa Chama cha Makandarasi Tanzania (CATA), Milton Nyerere, alisema ni wakati wa serikali kuzingatia kwa kuwapa zabuni makandarasi wa ndani, huku akizitaka kampuni za kigeni kubadilishana uzoefu na wenyeji.

"Ninatoa wito kwa watendaji wa wizara husika kuzingatia makandarasi wa ndani katika miradi ijayo ya kimkakati itakayofanyika hapa nchini," alisema.

Juni 15, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa mkoani Mwanza wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi ujenzi wa reli ya kisasa Mwanza hadi Isaka (34km), alitoa wito kwa Watanzania kulipa kodi ili kufanikisha ujenzi wa mradi huo na kwamba kukamilika kwa miradi hiyo ni chachu ya kukuza uchumi hususan sekta ya viwanda.

Miongoni mwa miradi ya kimkakati inayofanyika nchini ni ujenzi wa kituo cha umeme cha Mwalimu Julius Nyerere, reli ya kisasa (SGR), madaraja ya Tanzanite Dar es Salaam na Kigongo Busisi mkoani Mwanza.

# RC ampa kibarua DC kufuatilia madai watumishi kutishiwa maisha

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Peter Lijualikali, kufuatilia madai ya watumishi wa umma wa wilaya humo wanaodai kutishiwa maisha na watu wasiojulikana.

Agizo hilo alilitoa juzi muda mfupi baada ya kumwapisha kuwa Mkuu wa Wilaya ya Nkasi.

Alisema amepokea barua kutoka kwa watumishi wa wilaya hiyo wakimlalamikia kutishiwa maisha, kitendo kilichomshangaza kuona watumishi wa umma wanatishiwa maisha mpaka kwenda kulalamika na mifumo yote ya serikali ya wilaya ipo.

"Nimepokea barua kutoka kwa watumishi wa umma wilayani Nkasi wakidai kuwa wanatishiwa maisha, wakati serikali na mifumo yake yote ipo huko, Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Nkasi upo tu mpaka watumishi wanalalamika kwangu," alihoji na kuongeza.

"Nakuagiza mkuu wa wilaya nenda kafuatilie hili na uchukue hatua, haiwezekani watumishi wakaishi huko kwa hofu wakati serikali ipo nenda kahakikishe serikali na mifumo yake yote inafanya kazi," alisisitiza.

Aliwaagiza wakuu wa wilaya waliopangiwa kazi katika wilaya za mkoa huo kuhakikisha suala la kukusanya kodi linakua ni ajenda yao katika kipindi chote watakachokuwa wanafanya kazi katika wilaya zao.

Mkuu huyo wa wilaya alisema kuwa Rais wa Awamu ya Sita ameahidi kutekeleza miradi yote mikubwa ya kimkakati iliyoachwa na marehemu Dk. John Magufuli na kwamba fedha ni lazima ipatikane badala ya kutegemea mikopo, pia watumie makusanyo ya ndani.

Hata hivyo, alisema kuwa wakuu hao wa wilaya wana wajibu wa kusimamia makusanyo yatumike kama yalivyo kusudiwa na hataki kusikia watendaji wanatuhumiwa kula fedha mbichi za makusanyo katika kipindi chote atakachokua Mkuu wa Mkoa wa Rukwa.

# Wamlalamikia mkurugenzi kukaidi kuwapimia viwanja

**Na Richard Makore,** MWANZA

MKURUGENZI wa Jiji la Mwanza, Kiomoni Kibamba, anadaiwa kukaidi agizo la Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Ngusa Samike la kumtaka awapimie viwanja wananchi zaidi ya 143 wa Luchelele katika Wilaya ya Nyamagana.

Agizo hilo lilitolewa na Katibu Tawala huyo baada ya wananchi hao kwenda ofisini kwake kuomba utatuzi wa suala hilo siku chache kabla ya ziara ya siku tatu ya Rais Samia Suluhu Hassan, mkoani Mwanza iliyofanyika kati ya Juni 13 hadi Juni 15, mwaka huu.

Samike alimpigia simu Mkurugenzi huyo ambaye aliwasili ofisini kwake na kukiri kulifahamu suala hilo na kuahidi atalishughulikia na kulitatua.

Hata hivyo, juzi aliwaita wananchi hao ofisini kwake, lakini akashindwa kuonana nao.

Wakizungumza na waandishi katika ofisi za halmashauri ya jiji hilo, wananchi hao wa Luchelele ambao walikuwa wameenda kukutana na Mkurugenzi huyo kama walivyokubaliana, walitoa kilio chao kwa serikali kuingilia kati suala hilo liweze kumalizika.

Mwakilishi wa wananchi hao, Fortunatus Maiga, alisema upimaji wa maeneo ya Jiji la Mwanza siyo shirikishi kwa sababu tangu mwaka 2001 hadi 2003 wanazungushwa kupimiwa ama kufidia waondoke maeneo hayo.

Alisema maeneo hayo yalichukuliwa kwa ajili ya matumizi ya umma, lakini kwa sasa wanaona yanauzwa bila kufidiwa.

Maiga alisema halmashauri hiyo imebeba viwanja kupitia kitengo cha ardhi na kuwapa madalali ambao wakiviuza wanawapatia fedha.

Alisema wameishi hapo miaka mingi, lakini wanabomolewa nyumba zao bila kuwapa fidia.

"Maeneo yetu yamechukuliwa na jiji ukiona maeneo waliochukua na kuwapatia hao madalali utawaonea huruma na utajiuliza ni kwa manufaa ya umma au ya wafanyakazi wa jiji," alisema.

Aliiomba serikali kupitia kwa Rais, Waziri Mkuu na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kulitupia jicho la tatu na la kipekee halmashauri ya jiji la Mwanza ili liweze kutenda haki.

"Mwaka 2014 ulifanyika upimaji kwa sheria ya mipango miji, kwa hiyo wananchi wote wa kanda ya Luchelele, mpango wa halmashauri ya jiji ilikuwa ni kuwapa fedha chini ya kiwango kwa fidia ya hekari moja kwa Sh. milioni tatu ambacho walikipinga," alisema.

Mkazi mwingine wa Luchelele, Nkeziah Kayamba, alisema kuwa baada ya kuzungumza na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza wakati huo, Robert Chalamila, Mkurugenzi wa jiji alisema angependa kuonana nao baada ya ugeni wa rais kuondoka.

"Sasa sisi tuliobeba mzigo tunashindwa je, wenzetu wana hali gani ni kwamba watu hawaendelezi maeneo yao hawezi kufanya biashara na kujenga kwa sababu suala hilo halijafanyiwa utekelezaji," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Kiomoni Kibamba, alipotafutwa na waandishi alionyesha kulifahamu tatizo na kueleza kuwa baada ya Mwenge kupita Julai 7, ataenda katika eneo hilo la Luchelele.

"Nyie ndiyo wananchi wa Luchelele nitawapigia simu, leo sitoweza kuongea na nyie nina kikao cha maandalizi ya kupokea Mwenge au nitakuja huko Julai 7 au 8, "alisema.

Kuhusu agizo la Mkuu wa Mkoa la kumtaka awapimie ardhi wananchi hao, Kibamba hakujibu chochote na kuondoka huku akiwaacha wakazi hao wa Luchelele katika viwanja vya ofisi yake.




Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omari Kumbilamoto, akipokea zawadi kutoka kwa Mkurugenzi Mwendeshaji wa Benki ya Equity, Esther Kitoka, baada ya kufungua semina fupi jijini humo juzi, kuhusu bidhaa mpya ya benki hiyo kwa wafanyabiashara wadogo iitwayo Fanikisha Machinga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Tanzania kinara utengenezaji mabomba

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imekuwa nchi ya kwanza Afrika na ya 11 duniani kuanzisha teknolojia ya mabomba yenye kipenyo kikubwa ambayo ni suluhisho la muda mrefu la tatizo la miundombinu ya majisafi na majitaka nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Prof. Mkumbukwa Mtambo, wakati akizundua mwonekano mpya 'Brand identity' wa kampuni ya kuzalisha mabomba ya Plasco Limited.

Plasco ambayo ni wazalishaji wa mabomba ya maji, imezindua mwonekano huo ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia katika uzalishaji wa bidhaa na huduma katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Prof. Mtambo aliipongeza kampuni hiyo kwa kubadili mwonekano wake ambao unaonyesha ufanisi wa teknolojia yake mpya ya kisasa maarufu kama 'Weholite'.

"Inatia moyo kuona Tanzania inakuwa nchi ya kwanza katika bara la Afrika na ya 11 duniani kuanzisha teknolojia ya 'Weholite'. Teknolojia hiyo ni suluhisho la muda mrefu la changamoto za miundombinu ya majisafi na majitaka nchini," alisema.

"Sekta binafsi ni usukani wa kuendesha na kuongoza uchumi wa viwanda Tanzania na Plasco imethibitisha hilo. Ili kuwa nchi ya viwanda, tunahitaji aina hii ya viwanda ambavyo huzingatia ubunifu katika kuleta ushindani endelevu," aliongeza. Aliishauri kampuni hiyo kutafuta masoko mapya nje ya Tanzania ili kukuza uzalishaji na mtaji pamoja na kuongeza ajira.

Prof. Mtambo aliipongeza kampuni hiyo kwa kujenga maabara ya kupima ubora wa bidhaa ndani ya kiwanda hicho, tofauti na kampuni zingine ambazo hazizingatii kipengele hicho muhimu.

Uzinduzi huo umefanyika kwa kutumia kaulimbiu isemayo "We Stand for Quality" yaani tunasimamia ubora, ikidhihirisha uwezo wa kampuni hiyo katika kuzalisha bidhaa bora na zenye viwango vya kimataifa hapa nchini.

Ikiwa imeanzishwa takribani miongo mitatu iliyopita, Plasco Limited ni kampuni inayoongoza katika utengenezaji wa mabomba ya plastiki ikizalisha mabomba aina mbalimbali ikiwamo 'unplasticized polyvinyl-chloride (uPVC)', 'High Density Polyethylene (HDPE)' na mabomba aina ya 'Weholite HDPE' ambayo ni teknolojia ya kisasa zaidi.

Ofisa Uendeshaji Mkuu wa Plasco Limited, Alimiya Osman, alisema: "Imekuwa safari ndefu ya kujenga kampuni yetu na tumeamua kufanya mabadiliko kuendana na mageuzi ya teknolojia kwenye sekta hii. Tumejizatiti kuzalisha bidhaa bora na zenye viwango vya kimataifa ambazo zinaweza kudumu kwa muda mrefu."

# Serikali yaahidi ujenzi barabara Magu

SERIKALI imesema itaendelea na ujenzi wa barabara ya Magu hadi Ng'hungumalwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Magu (CCM), Boniventura Kiswaga.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini ujenzi wa barabara ya Magu – Ng'hungumalwa kwa kiwango cha lami utaanza baada ya upembuzi yakinifu kukamilika.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alisema kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Magu – Bukwimba - Ngudu – Ng'hungumalwa yenye urefu wa kilometa 71 ilikamilika mwaka 2019.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali imetenga Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilometa 10 katika barabara hiyo.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Nyang'hwale, Hussein Amri, alisema kwa kuwa serikali ilishapitisha ujenzi wa barabara kutoka Geita hadi Nyang'hwale na kwamba kila mwaka zimekuwa zikijengwa kwa kilometa nne lakini mwaka huu fedha hazijapelekwa. Kutokana na hali hiyo, mbunge huyo alihoji serikali inatoa kauli gani kuhusu ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema serikali imeshaanza kujenga barabara hiyo na haijaifuta kuijenga kwa kiwango cha lami.

"Nimhakikishie mbunge kuwa barabara hii itaendelea kujengwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo haijafutwa na hakuna mpango wa kuifuta," alisema.



Mkalimani wa lugha za alama (kushoto), akiwatafsiria baadhi ya wenye ulemavu wa kusikia (viziwi), waliotembelea Bungeni, jijini Dodoma jana, kujifunza shughuli za bunge. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Maombi wilaya mpya Ukonga bado

BUNGE limeelezwa kuwa Wilaya ya Ilala bado haijawasilisha maombi ya kuanzishwa kwa wilaya mpya ya Ukonga kwa mujibu wa matakwa ya sheria.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariam Kisangi.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuanzisha wilaya mpya ya Ukonga katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Silinde alisema eneo la Ukonga liko katika Wilaya ya Ilala ambayo ni moja kati ya wilaya tano zinazounda Mkoa wa Dar es Salaam.

Silinde alisema utaratibu wa kuanzisha mkoa na wilaya mpya umebainishwa kupitia sheria ya uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya namba 397 ya mwaka 2020.

Alibainisha utaratibu wa kuanzisha wilaya mpya huanzia kwenye serikali za vijiji au mitaa ili kupata ridhaa ya wananchi kisha hupelekwa kwenye mabaraza ya madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

"Baada ya hatua hiyo, maombi hayo huwasilishwa Ofisi ya Rais -TAMISEMI kwa ajili ya uhakiki na kujiridhisha na baadaye kuwasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maamuzi (uamuzi)," alisema.

Silinde alisema kama kuna maombi mapya ni lazima mchakato uanze upya na kwamba maombi ya nyuma kwa sasa hayatambuliki.

"Kwa sababu zoezi (kazi) lile (ile) lilifanyika (ilishafanyika) kwa wakati mmoja na wilaya zilizokidhi vigezo zilianzishwa, ushauri wangu anzeni upya watu wa Ukonga na tutaamua kulingana na matakwa ya kisheria kama kupeleka kwa Rais ili atoe uamuzi wa mwisho wa kuanzisha au kusitisha," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Makambako (CCM), Deo Sanga, alihoji serikali haioni sababu ya kuitambua Makambako kama wilaya kutokana na taasisi zingine muundo wake kuitambua kiwilaya.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema endapo wanaona kama wanahitaji kuwa wilaya wafuate taratibu za kisheria.

Hata hivyo, Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alishauri mgawanyo wa maeneo ya kiutawala ni vyema wakati wa kujiridhisha yakazingatia jiografia ya maeneo husika ili kuleta uwiano wa kutoa huduma.

# Mbunge alia uhaba dawa

MBUNGE wa Ulanga (CCM), Alaudin Salim, amehoji serikali ina mpango gani wa kutatua ukosefu wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya wilayani Ulanga.


Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mitaa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema serikali imeendelea kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa kuongeza bajeti katika wilaya ya Ulanga na nchini kote.

Alisema bajeti ya dawa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga imeongezeka kutoka Sh. milioni 337.49 (serikali kuu, fedha uchangiaji huduma na Mfuko wa Pamoja wa Afya) mwaka 2015/16 hadi Sh. milioni 475.53 mwaka 2020/21.

Alibainisha kuwa upatikanaji wa dawa muhimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga umeongezeka kutoka asilimia 68 mwaka 2015/16 hadi asilimia 82.2 mwaka 2020/21.

Alisema pamoja na jitihada hizi bado kuna upungufu wa baadhi ya dawa na vifaa tiba vituoni.

"Serikali itaendelea kuboresha bajeti na usimamizi wa bidhaa hizi ili kuondoa changamoto hiyo," alisema.






Ukurasa 13

Madisii mkipandisha mabega mmezinguliwa



Ukurasa 14

**NDOA, MAMA KUMTUNZA KIJANA...**
**Shida ya ajira na kuendekeza 'dezo'chanzo kushamiri tabia kila kukicha**

BUFE
IJUMAA JUNI 25, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

NEEMA NDANI YA WIKI YA UTUMISHI...

# REA yaanza Mtwara Awamu Tatu kuneemesha umeme kwa vijiji 300

**Na Yasmine Protace**

HADI sasa mradi wa kufikisha umeme vijijini nchini, au REA utekelezaji wake uko katika Awamu ya Tatu.

Tafsiri ya kuundwa na kupiganiwa mradi huo, ni kwamba umeme unapokuwapo unasaidia kupunguzia wananchi gharama na kero za mahitaji, zikiwamo kuchaji simu, kusaga nafaka na kupunguzia matumizi ya umeme wa jenereta.

Umeme una msaada mkubwa katika maendeleo kwa umma, kwani hata katika vituo vya afya na zahanati unahitajika mno.

Hivi karibuni, Waziri wa Nishati Dk. Medard Kalemani, amezindua Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Mtwara, unaolenga kufikisha umemekatika vijiji vyote vilivyosalia vya Mkoa huo.

Dk. Kalemani alizindua mradi huo Juni 19 mwaka huu katika kijiji cha Namtumbuka, Mtwara Vijijini aliambatana na watu mbalimbali. Ni ndio ilikuwa mahsusi ndani Wiki ya Utumishi wa Umma.

Baadhi ya watu walioambatana na waziri, ni Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Dunstan Kyobya, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa.

Wengine ni wabunge, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Wakili Julius Kalolo, Mjumbe wa Bodi hiyo, Oswald Urasa, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Wakala, Mhandisi Jones Olotu, viongozi na wataalam wa REA na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).



Waziri wa Nishati Dk. Medard Kalemani (katikati), akikata utepe kuashiria kuzindua rasmi Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Mtwara. Uzinduzi huo ulifanyika katika kijiji cha Namtumbuka, Mtwara Vijijini, Juni 19, 2021. **PICHA: MTANDAO.**

Akizungumza na wananchi wakati wa hafla hiyo ya uzinduzi, Waziri Dk. Kalemani, alieleza lengo la mradi husika ni kufikisha umeme katika vijiji 384 vya Mkoa wa Mtwara, ambavyo havijafikiwa na nishati hiyo.

"Mkoa wa Mtwara una vijiji vyenye umeme 413, kati ya 797. Kwa kutambua hilo, leo ninawakabidhi makandarasi wasimamie mkoa huu kwa pamoja na kuhakikisha vijiji vyote vilivyosalia vinapatiwa umeme katika mradi huu," anasema.

Anautaja mradi umefadhiliwa na serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na anawataka wananchi wa Mtwara kuutumia katika shughuli za maendeleo kuboresha maisha yao na uchumi nchi jumla.

**KUTOKA REA**

Mwenyekiti wa Bodi ya REAtearea, Wakili Kalolo aansema wameandaa mpango kazi wa miaka mitano, uliojikita katika kufanikisha malengo ya serikali ya kusambaza nishati ya umeme katika vijiji vyote ifikapo Desemba mwaka ujao na vitongoji vyote mwaka 2025.

Anasema, ni mpango unaolenga kufikisha umeme viwandani, kwenye madini, kilimo, uvuvi na ufugaji. Anafafanua: "Mradi huu unaouzindua leo ni sehemu tu ya Mpango Mkakati wa Wakala na umelenga kusambaza umeme katika vijiji 1956 ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme."

Anasema kuwa nmradi utatekelezwa katika mikoa 24 na imegawanywa katika makundi 39 yanayokadiriwa kugharimu takribani Sh. trilioni 1.3 na utakamilika Desemba mwaka ujao.

Wakili Kalolo anaongeza kuwa, mradi utakapokamilika utawezesha vijiji vyote 12,268 nchini kupatiwa umeme na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kwa Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara, kufikisha umeme katika vijiji vyake vyote.

Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi kutoka REA, Mhandisi, Jones Olotu, aliyemwakilisha Mkurugenzi wa wakala, alieleza kuwa katika Mradi huo mkoani Mtwara, wateja wa awali 6,182 wataunganishwa.

Anasema, utekelezaji wa mradi katika Mkoa huo utagharimu Sh. bilioni 62.146 na utatekelezwa na mkandarasi aliyeteuliwa katika wilaya za Masasi na Nanyumbu na mkandarasi mwingine, katika wilaya za Mtwara Vijijini, Newala na Tandahimba.

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Dunstan Kyobya, anasema umeme una umuhimu wa pekee katika Mkoa wa Mtwara, kwa taswira za kimaendeleo, oia usalama wa nchi.

Wabunge mashuhuda na waliozungumza wanajumuisha: Geofrey Mwambe (Ndanda), Issa Mchungahela (Lulindi), Katani Katani (Tandahimba), Hassan Mtenga (Mtwara Mjini) na Abdallah Chikota (Nanyamba), wote walipongeza jitihada zinazofanywa na serikali.

Waliwataka makandarasi waliopewa dhamana ya kutekeleza mradi husika kwa kuhakikisha wanafanya kazi hiyo kwa uaminifu na weledi huku wakiwahakikishia kuwa watawasimamia ipasavyo ili wasiiangushe serikali na wananchi wao.

UCHUMI

## WIKI YA UTUMISHI 2021

# Wizara ya Ardhi yatekeleza kwa ziara maalum halmashauri zote mikoa Lindi, Mtwara, Ruvuma

## •Yasafisha ‘makandokando’ kuleta maisha mapya

**Na Munir Shemweta**

KILA tarehe 16 hadi 23 ya mwezi huu kila mwaka, nchini Tanzania na duniani, kunaadhimishwa Wiki ya Utumishi wa Umma.

Ni kawaida yake, tukio hilo linaandamana na shughuli zinazohusu utumishi wa ufanyaji kazi za umma. Hapo hupambwa na maonyesho ya shughuli za wizara na taasisi za umma zinazoshiriki kuonyesha huduma zao, sambamba na kuwahudumia wananchi.

Mwaka huu kila wizara na taasisi zimejiwekea utaratibu wa kuadhimisha wiki hiyo, ingawa ni kwa kuzingatia kaulimbiu ya maadhimisho hayo na kauli mbiu ya mwaka huu ni Kujenga Afrika tunayoitaka, kupitia utamaduni wa uadilifu unaostawisha uongozi wenye maono hata katika mazingira ya mgogoro.”

Baadhi ya wizara na taasisi za umma katika maadhimisho ya mwaka huu, ziliamua kuendeleza utaratibu wa kukutana na watumishi wake kwa kusikiliza na kuzipatia ufumbuzi magumu ya watumishi wake.



Waziri mwenye dhamana na sekta ya Ardhi, William Lukuvi, alipokuwa katika moja ya matukio ya kikazi mkoani Lindi. **PICHA: MTANDAO**

**UTEKELEZAJI WIZARANI**

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, iliamua kuja tofauti katika kuadhimisha wiki hiyo kwa maofisa wake kutoka makao makuu ya wizara kutembelea ofisi zilizoko pembezoni, kwa lengo la kusikiliza na kuzipatia ufumbuzi kero na mikwamo za watumishi wake walioko huko.

Utaratibu uliofanywa na Wizara ya Ardhi una mtazamo wa kwanza kutambua kazi zinazofanywa na watumishi hao wa pembezoni, pia kufuatilia na kutathmini changamoto zinazowakabili kwa mitazamo yao wanaonekana kama ‘wametengwa.’

Mara kadhaa kumejengeka dhana kwamba, matendo ya watumishi kuhamishiwa maeneo ya pembezoni, basi ama wanatafuta njia ya kubatilisha uhamisho ili kurejea mjini au visingizo mbalimbali ikiwamo ugonjwa, kwa lengo la kukwepa kwenda kufanya kazi maeneo hayo.

Wizara ya Ardhi ikaona haja ya kutibu hilo, ikianzia na kutafuta namna bora ya kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi changamoto za watumishi waliopo kwenye ofisi za pembezoni, ili nao waone fahari kufanya kazi katika mazingira na utashi kama uleule wa wenzao wa makao makuu.

Kupitia Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ya mwaka huu wa 2021 watumishi wa sekta ya ardhi katika mikoa iliyotembelewa walipata fursa ya kuwasilisha changamoto mbalimbali zinazowakabili maeneo yao ya kazi.

**RUVUMA**

Msisitizo mkubwa wa maofisa wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, waliotembelea ofisi zao katika mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi, ilijumuisha usikilizaji shida zao na kuwataka watendaji wa sekta ya ardhi kuhakikisha wanashirikiana na kuacha tofauti kwenye utendaji kazi, ili kuleta ufanisi na tija katika sekta hiyo.

Ofisa Utumishi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mwajabu Masimba, aliyeongoza timu hiyo ya maofisa watatu kutoka wizarani, kwenda kufanya ziara hiyo.

Huko amewaambia watumishi wa sekta ya ardhi kwa nyakati tofauti kwenye mikoa hiyo, kwamba hawatakiwi kutofautiana kiutendaji wao wa kazi, hata kama ni wa kada tofauti, kwani ni hali inayozalisha tija kwenye sekta ardhi.

Kwa mujibu wa Mwajabu, kufanya kazi maeneo ya pembezo si hakumaaanishi wamewatenga watumishi wa maeneo hayo, bali ni sehemu ya majukumu, ikibeba maana ya Wizara ya Ardhi kuamua kupeleka timu ya maofisa wake kujua na kuzipatia ufumbuzi changamoto zao.

“Tushirikiane kila moja kwa kazi yake na mkumbuke muda mwingi tunautumia ofisini, hivyo ushirikiano mtakaofanya kwenye utendaji kazi na kuondoa tofauti utaifanya wizara kusonga mbele kwa kuwa taswira nzuri ya ofisi inajengwa na watumishi,” anasema Mwajabu.

Ofisa Mipango Miji kutoka Idara ya Maendeleo ya Mkazi wizarani, Emile Mwasyoge, anawatia moyo watumishi wa sekta ya ardhi mkoani Ruvuma, wasirudishwe nyuma na magumu kikazi na akawapa silaha ya uvumilivu ndio nyenzo ya kuwainua.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoa wa Ruvuma, Ildefonce Ndemela, anawakumbusha watumishi wa sekta ya ardhi mkoani kwake wahakikishe wanatimiza wajibu wao, wakati kuna changamoto zinazofanyiwa kazi na ngazi za juu.

Watumishi wa Sekta ya Ardhi mkoani Ruvuma, walieleza changamoto za kiutendaji na binafsi zinazowakabili katika maeneo yao, ambako baadhi yake ni upungufu wa watumishi na vifaa vya kazi kama vile magari.

**MTWARA**

Mkoani Mtwara, timu hiyo ya wizara, mbali na maofisa Mwajabu na Elime, pia alikuwapo ofisa kutoka Idara ya Upimaji na Ramani Siri Mrisho, ambako walisikiliza na na kupokea taarifa za magumu, pia ushauri wa watumishi mkoani humo kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na sekta kwa ujumla.

Watumishi wa Sekta ya Ardhi katika mikoa iliyotembelewa, walipongeza hatua ya Wizara ya Ardhi kuwafuata watumishi waliko kujua yanayowakwaza kikazi, kukiwamo madai na hata ya dodoso za uthibitisho kuwapo watumishi wanaofanya kazi maeneo ya pembezoni wanasahaulika, hata wanajihisi wametengwa.

“Utaratibu uliofanywa na wizara safari hii, kipindi hiki cha Wiki ya Utumishi wa Umma, unatakiwa uwe endelevu kwa kuwa watumishi wanaofanya kazi pembezoni wanazo changamoto nyingi, ukilinganisha na wanaofanya kazi maeneo mengine,” anatamka Daniel Nguno, Ofisa Mipango Miji wa Mkoa Mtwara.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mtwara, Rehema Mwinuka, anashukuru ziara yake kwenye mikoa ya pembezoni, akieleza faraja ya mkoa wake kuwa miongoni mwa michache iliotembelewa, kati ya mikoa yote kitaifa.

Ni ziara ambayo mzunguko wake haukuishia makoa makuu ya mkoa pekee, bali ilizama hadi kwenye halmashauri zote za wilaya, miji na manispaa za mikoa hiyo mitatu, Lindi, Mtwara na Ruvuma.

**WAJIBU WA WIZARA**

Miaka kadhaa iliyopita, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ilifanya mageuzi makubwa ya kiutendaji kwa kuhamishia watumishi wake wote waliokuwa wanawajibikia majukumu ya sekta hiyo, kutoka kwenye serikali za mitaa wakiwa chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na kuhamia wizara ya sekta yao, wanakotuimikia hadi sasa.

**Majukumu yao makuu ni yafuatayo:**

- Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi;
- Kusimamia upangaji wa miji na vijiji;
- Kupima ardhi na kutayarisha ramani;
- Kutoa hati za kumiliki ardhi na hatimiliki za kimila;
- Kusajili hati za umiliki ardhi na nyaraka za kisheria;
- Kuthamini mali;
- Kuhamasisha na kuwezesha wananchi kuwa na nyumba bora;
- Kutatua migogoro ya ardhi na nyumba;
- Kusimamia upatikanaji na utunzaji wa kumbukumbu za ardhi;
- Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na huduma za sekta ya ardhi;
- Kusimamia Shirika la Nyumba la Taifa, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi na Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni;
- Kusimamia uendeshaji wa Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro; na,
- Kusimamia maslahi na utendaji kazi wa watumishi wa sekta ya ardhi




Ofisa Utumishi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mwajabu Masimba, akizungumza na watumishi wa Sekta ya Ardhi mkoani wa Lindi.



Mmoja wa Watumishi wa Sekta ya Ardhi katika mkoa wa Ruvuma, alipowasilisha matatizo ya kazi waliyonayo, pindi walipotembelewa na maofisa wa makao makuu. **PICHA ZOTE: MUNIR SHEMWETA**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Madisii mkipandisha mabega mmezinguliwa






**NA JOSEPH KULANGWA**
+255 713 410008

UKITAKA kujua matatizo ya dunia hii, basi uishi katika ulimwengu wa kambo. Uishi katika familia yenye watoto au wazazi wa kambo. Humo utashuhudia mambo mengi usiyotarajia, lakini makubwa yakijikita kwenye ubaguzi.

Kwa wazazi, unaweza usione sana, lakini yatajitokeza zaidi kwa watoto ambao hutegemea wazazi wawachukulie poa kama ndugu, lakini watoto hubaki kujishuku kila mara, kwamba kwa kuwa si watoto wa mmoja wao basi kuna kijiubaguzi.

Wazazi mara nyingi kama si wote, hujua majukumu yao ni kulea watoto hata kama hawakuwazaa wao. Ukikuta katika familia kuna mzazi mmoja anabagua mtoto wa mume au mke, ujue kuna tatizo.

Kama mume au mke huyo si mlevi, basi ni mwezi mchanga, si bure. Ni kwanini? ni kwa sababu mzazi kama mzazi hatakiwi kabisa kuonyesha upendeleo, kwa kuwa tu hana unasaba na mtoto mmoja, wawili au wote, kwa kuwa tu hakuwazaa.

Ubaguzi kama huu ulishasababisha baadhi ya watoto kuteswa na kuwekwa ulemavu, kama si kuuawa. Ubaguzi wa kiwango hicho hubaki kuwa dhambi tu kwa Mungu na afanyaye hayo husubiri adhabu yake kiyama.

Haya mambo ya ukambo yalishafika hata kwenye jamii mbalimbali, zikiwamo hizi za kisiasa ambako katika mataifa yetu haya, kuna imani za mifumo ya vyama vingi vya siasa, ambako mpinzani huonekana adui na mtawala hasimu.

Sina sababu ya kusahau, mwaka 2015 ambao meti wangu Dk. John Magufuli aliingia madarakani, akaenda Pemba na akamshangaa Dokta mwenziwe, Ali Mohamed Shein kuteua mpinzani katika serikali yake, akisema angekuwa yeye asingethubutu!

Mimi nikajua tu ndugu yangu alikuwa bado ana moto wa utashi wa kampeni za uchaguzi, ambako alibadilishana maneno makali na mazito na wapinzani akichuana na Edo Lowassa kutwaa nchi, ingawa wao kama wao hawakusilibiana.

Mara zote waliwaachia wapambe wao kusiliba, lakini wawili hao wakiwa mahasimu kwa wakati huo, wakipuyanga kuomba kura kwa wananchi na kuwaachia wajuao majukwaa kujinasibu kwa niaba yao na wakaangukia vifaulo vya hapa na pale.

Lakini kidogo kidogo, moto wa utashi ulipopoa kichwani, tukaanza kuona akiteua. Akaanza na Anna Mghwira wa ACT-Wazalendo, akimpa ukuu wa mkoa wa Kilimanjaro, tukidhani ameishia hapo, mara tukamsikia Kitila Mkumbo, mara Kafulila na wengineo. Tukajua tu mambo sasa shwari.

Tukaenda nao huku wakibadili itikadi zao kimya kimya, mara ukafika uchaguzi mkuu mwaka jana, zikaibuka tena kauli za ‘ukichagua upinzani hakuna maendeleo’.

Dk, Magu alipoaga dunia, akaingia Rais Samia Suluhu Hassan, huyu akaingia na huruma, akaja na upendo wa dhati wa mama, akasema hataona muhali kuteua mtu kutoka itikadi nyingine, ili mradi anachapa kazi ya kusaidia Watanzania kwa kuwa nchi ni ya Watanzania.

Wakidhani anatania, akaona athibitishe kwa kuanza na Queen Sendiga kutoka ADC, akambandika ukuu wa mkoa wa Iringa, vicheko na vilio vikapita. Akaenda kuzungumza na mayanki Mwanza, akawaambia “nitakunjua mkeka na mtakuwamo tu msiwe na shaka na mimi.”

Alipoukunjua, wapinzani kibao, wasanii kibao, wanahabari kibao. Lakini, jicho likakodolea kunako wapinzani zaidi. Kuna walio ndani ya Chama Tawala wakaibuka wakiguna, oh inakuwaje sasa! Tulipigania chama tukikesha nje sasa vipi!

Oh sisi tulivunjika mikono, tulitukanwa na wapinzani, tulinusurika kuuawa, waliouawa je, wakikipigania Chama mbona hawasomeki kwenye mkeka, inakuwaje sasa? Mwenye ‘plate number’ yake ninayompa SSH akatulia kimya akiwaangalia tu na kujiuliza, “kwani hawakunielewa Mwanza?”

Vilio hivi vya Sisiemu wanaowaona wapinzani wana wa kambo ni ujumbe kwa walioteuliwa, kupiga mzigo mpaka Mama aone “yes sikufanya makosa”, lakini wajue wakimzingua, palepale atawazingua. Jiulize, wako wapi kina naniliu hawa waliokuwa wanasemasema sana?

Ninyi vijana madisii, msiende huko mkajisahau mkatanguliza ugeni wenu wa mtaa wa uongozi, mkapandisha mabega, mkatukana wazee wenu kwa hayo makali yasiyotamkika... kaeni chonjo, SSH hatasita kukuzingueni nakwambieni! Alamsiki!

UCHUMI

NDOA YA MAMA KUMTUNZA KIJANA...

# Shida ya ajira na kuendekeza 'dezo' chanzo kushamiri tabia kila kukicha

## •Mageuzi mila, mfumo madaraka yana yake

**Martha Mwasyeba na Zuwena Shame**



Namna zilivyo ndoa za umri tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

KUNA hoja katika jamii, kwamba kutoweka kwa jando na unyago au wazazi wanapokosa muda wa kukaa na vijana wao wa kiume kuwaasa

Ndani ya hilo, kuna kidole wananyooshewa kwamba ni woga na wavivu kimaisha katika vyanzo vya kutafuta riziki, kwamba inasababisha wimbi la vijana wanaohamia kulelewa na kinamama waliowazidi umri, jambo lisilo sahihi kimila.

Sasa kuna maswali yanyotawala, je ni jadi ya jamii iliyoko kukuza mwenendo waliorithi kihistoria? Nipashe iliamua kufanya dodoso kutoka vyanzo mbalimbali vya habari kwa vijana wahusika kutoa majibu.

**WANALOSEMA WAZEE**

Godfrey Lugalambi kutoka Pugu, nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam, ana maoni: "Vijana wengi kutojielewa na kujua wajibu wao, ndio inasababisha wengi kutamani kulelewa ili kulazimisha maisha yawe mepesi.

"Lakini, tofauti ni kwamba uhusiano wao unakuwa hauna uhuru wala ujasiri kama wanaume matokeo yao 'hupelekeshwa' na kulazimishwa kufanya mambo ambayo ni kinyume na matakwa yao."

Ndani ya mustakabali huo, kunatajwa ugumu wa maisha na kukosa ajira, kunawasukuma vijana kuingia ubia wa kimapenzi na waliowazidi umri, unaowaacha katika uvivu wa kujimudu kiuchumi, wanajiegesha penye hatima ya pato, ili kuwasaidia kimaisha.

Sura ya pili ni mtazamo unaozama kihisia zaidi kwenye mustakabali wa mapenzi kijamii; huku

jingine kuna maendeleo, nafasi kubwa ya kikazi sasa zinashikiliwa na wanawake kukuza uwiano wa fursa kazini kwa wanawake na taasisi nyingi ziko chini ya wanawake na zina kundi kubwa la wanawake.

Hata hivyo, kitaalamu inataja kusahauliwa dhana kwamba namna mwanamke atakavyoathiriwa, katika namna moja na nyingine.

Mathias Philipo, anawataja vijana kuathiriwa na shida ya ajira, sambamba na utamaduni wa uvivu, wamekata tamaa na ama kujishughulisha au wanasubiri kuajiriwa.

Hapo ndipo dhana ya maisha rahisi kupitia kulelewa na kinamama inapozaliwa. Anasema, ingawaje jambo geni katika jamii ya nchini, kwa mataifa mengine ni utamaduni wa kawaida.

Mitandao ya kijamii kwa upande mwingine, inatajwa kuchangia sana kuwahamasiha wanaooa na kuolewa wanaiga maisha ya nchi nyinginezo kujituma kwa kusaka kipato.

Vilevile, wanatajwa vijana wengi kutamani maisha makubwa pasipo uwezo wa kuyamudu, hata wanaishia kutafuta wanawake walio na uwezo kiuchumi, wayafikie maisha bora, bila kuzingatia ama umri au dhana mbaya katika jamii inayowazunguka.

Anasema vijana wa kiume wanapokosa kazi, ni pengo kubwa hali inayowasogeza karibu na uhusaino kwa kinamama wenye pesa

Said Amour, mkazi wa Mbezi Makabe anachangia mada hiyo kwamba: "Wanawake wengi katika karne hii wanajiweza kiuchumi na wanatamani wapate kitu kinachowafurahisha.

"Kwa hiyo, wako tayari kutumia pesa zao ili kupata mwanamume yoyote wa kumfurahisha na kwa kuwa vijana ndio wenye nguvu na bado kiuchumi hawajakaa vizuri wako tayari kuwa na mtu mzima ili tu aweze kumsaidia kiuchumi."

Mzee Athumani Nguogani, kutoka Mtoni Kijichi jijini Dar es Salaam, anasema zamani jamii katika undugu wa kaya moja kwa upendo huku masuala ya kimila kama jando walifundishwa thamani ya kuwa wanaume na majukumu yao.

Anasema, hilo lilikuwa gumu kuona kijana akitamani maisha ya mteremko, tofauti na vijana wa kizazi cha sasa, mara nyingi wanajilea wenyewe kwa kuwa wazazi wengi wametingwa na majukumu na kusahau wajibu wa kuzungumza na vijana.

Ni matokeo wanayosema kijana analelewa na mitandao na televisheni na kuiga utamaduni ambao haujazoeleka kuishi na wanawake wenye umri sawa na mama zao.

Kwa mujibu wa Mzee Athumani, hoja hiyo hupewa jibu la 'umri ni namba tu' kwa hiyo hauwezi kuwazuia katikia maisha yaliyo mafupi na matamu, kuliko maisha marefu yenye tabu.

Anayejitambulisha jina la Mama Anna, anadokeza sababu ya kuongezeka wimbi hilo kubwa la vijana wanaopenda kulelewa na kinamama watu wazima, malezi anayoyaita mabaya ya wazazi na watoto hawajaandaliwa ipasavyo kuwa baba na familia baadaye.

Lingine analitaja ni kundi kubwa la watoto wanaolelewa na mzazi mmoja wa kike, maarufu kwa Wazungu 'single mother' linazidi kuongezeka, watoto wakikariri dhana mama ndio wenye jukumu la kulea familia.

Kupitia dhana hiyo anasema, inapotokea mwanamke anashawishi kijana asiye na kazi kwa hongo la kiuchumi, anakuwa yu tayari anamhitaji kumuhonga zawadi anakubali kirahisi, katika tafisri ya kupewa uwezo kiuchumi kwenda nyumbani kumhudumia mama.

Kinyume chake, Sophia anataja kinamama wengi baada ya kutumia muda mrefu masomoni wakiweka kando suala la ndoa, inafika wakat wanahitaji ndoa, inakuwa imewapita na wanaishia kutafuta vijana wasijiweza kiuchumi wakipitia pesa kuwanasa, hali inayoua hatima ya vijana hao.

**NAMNA YA KUJIZUIA**

Nini Kifanyike? Rai ya Sophia ni kwa wazazi watoe elimu kwa vijana kuwaambia uhumimu wa kujitegemea na kutafuta pesa kwa jasho lao, pasipo kuegemea pesa za wanawake wa umri mkubwa.

Hiyo inajumuishwa na hatua ya vijana kutambua majukumu yao katika jamii, fikra zao zielewe majukumu yao ya msingi ambayo hayakwepeki katika maisha, kwani athari ya kuyakwepa wanaishia kudharaulika katika jamii, kwa kanuni "hakuna baba mzigo katika familia atakayeheshimika."

Ni dhana inayotafisiriwa, pia katika maisha ya jamii yasikwepeke, kwamba wanawake wanaotumia pesa wanarubuni vijana wadogo wanaostahili kuwa na watoto, wanapunguza heshima ya neno mama katika jamii, hali inayoendana na uchumi wake.





## Majaliwa mgeni maadhimisho ya dawa za kulevya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa anatarajiwa kesho kuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya ambayo yatafanyika jijini Dodoma.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Gerald Kusaya, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema Tanzania inaendelea kupambana na dawa hizo huku akisisitiza haijaruhusu wananchi kulima bangi kama mazao mengine.

"Mazao ya biashara nchini tunayo zaidi ya 95. Ukichukua alizeti pekee yake tu bado hatujalima vya kutosha ndiyo maana leo hii taifa linaagiza mafuta ya kula kutoka nje na kutumia Sh. bilioni 500 kila mwaka. Pia bado yapo mahitaji ya shayiri lakini Misri wanahitaji pia mahindi ya njano," alisema Kusaya

"Hii bangi hata ikiruhusiwa leo si kila mtu atalima labda taasisi fulani ndiyo itahusika lakini pia hata hayo mataifa mengine yanayolima bangi si kama hii ambayo inaharibu akili za watu," alisisitiza.

Akizungumzia kuhusu hali ya udhibiti wa dawa za kulenya nchini, Kusaya alisema nchi iko katika kiwango kizuri cha mapambano dhidi ya mihadarati.

"Sisi kama taifa viko vyombo ambavyo viko juu yetu vinavyotuangalia na kututathimini tumefanya kwa kiasi gani kudhibiti matumizi pamoja na usambazwaji wa dawa hizi. Kwa mujibu wa ripoti ya mwaka 2019/20, Tanzania tumedhibiti dawa za kulevya kwa zaidi ya asilimia 90.

"Hivyo utaona kuwa tuko katika hatua nzuri lakini pia hivi sasa toka nimeingia madarakani tumeweka uangalizi wa juu sana ndiyo maana tulifanikiwa kukamata kiasi kikubwa sana cha dawa toka tupate uhuru ambacho ni kilo 856.39 za dawa za kulevya," alisema Kusaya.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, aliwataka wakazi wa mkoa huo kujitokeza kwa wingi katika maadhimisho hayo yatakayofanyika Viwanja vya Nyerere Square.

"Wananchi waje kwa wingi kwakuwa kutakuwapo na utoaji wa elimu mbalimbali juu ya athari za utumiaji wa dawa za kulevya kuanzia Juni 24 na maonyesho ya wajasiriamali mbalimbali kabla ya kilele," alisema.

# Wavuvi walia uhaba wa samaki Mtera

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

WAVUVI na wachuuzi wa samaki katika bwawa la Mtera, wamehamia mikoa mingine yenye mabwawa kutokana na uhaba wa samaki.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na waandishi wa habari kwenye kambi za wavuvi za Mapera Mengi, Chadumbwi na Migoli, walisema pamoja na kuwapo kwa maji mengi bado upatikanaji wa samaki umekuwa mgumu, hivyo kuathiri shughuli zao kiuchumi.

Jacob Mwalukali, mmoja wa wavuvi hao, alisema kutokana na hali hiyo, wakazi wengi wanaojishughulisha na uvuvi wamelazimika kufuata samaki kwenye maeneo mengine kama vile mikoa ya Singida, Kilimanjaro Arusha na wilayani Bahi.

Pia alisema uvuvi haramu ndani ya bwawa hilo, umechangia kuadimika kwa kitoweo hicho.

Simon Lukui kutoka kambi ya Migoli alisema hali hiyo imeathiri kushindwa kuhudumia watoto wao mahitaji ya shule na matibabu.

"Maji yamejaa kwenye bwawa letu lakini cha kushangaza samaki hakuna. Hawa mnaowaona wanatoka kwenye bwawa lililopo huko Bahi Nagulo na wengine wanatoka mikoa ya Singida, Arusha na Kilimanjaro," alisema Lukui.

Mshauri Mkuu wa Umoja wa Makanisa ya Kipentekoste Mtera, Askofu Mstaafu Aswelle Mwandamo, aliwataka wakazi wanaoishi kwenye kambi zilizoko kando kando ya bwawa hilo kudhibiti uvuvi haramu badala ya kuliacha suala hilo mikononi mwa serikali.

Alisema wajibu wa serikali ni kutoa elimu lakini wavuvi wajibu wao ni kushiriki kudhibiti ili kulinda rasilimali hiyo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (kulia) na akikabidhiwa kitabu cha taarifa ya hali ya dawa za kulevya ya mwaka 2020 na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Nchini, Gerald Kusaya, baada ya kuzungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# SMT, SMZ zakubaliana kutumia mfumo mpya utatuzi kero za maji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, zimeingia makubaliano ya kutumia mfumo mpya wa teknolojia ili kutatua kero za maji.

Makubaliano hayo yalifikiwa jijini Dodoma na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso na Waziri wa Maji na Nishati Zanzibar, Suleiman Masoud Makame, baada ya serikali hizo kujadili kero zilizomo kwenye sekta hiyo.

Katika mazungumzo yao, mawaziri hao waliweka bayana kuwa dhamira ya serikali ni kufikia malengo katika kutatua kero ya maji nchini.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Waziri Aweso alisema dhamira hiyo ni kuhakikisha serikali inamtua mama ndoo kichwani.

Katika kutimiza hilo, alisema wamezindua na kukagua moja ya mifumo hiyo mipya ambayo imeanza kufanya kazi katika majaribio ya utoaji wa hudumua kwa wateja.

"Dhima ya serikali katika mfumo huo mpya ni kuhakikisha wateja wote wa maji watatumia huduma ili kuepuka malalamiko ya kubambikiziwa bili kubwa," alisema.

"Sifa za mfumo huu zitamrahisishia mteja kupata huduma kwa haraka ikiwa ni pamoja na mteja kununua maji kwa simu ya mkononi, kuhama nyumba na 'unit' na kumhamishia mteja mwingine 'unit' za maji na kutambua kiwango cha maji yanayotumika kupitia simu ya mkononi."

Pia alisema makubaliano hayo yanalenga kutoa fursa kwa wizara hizo mbili zenye dhamana ya kutoa huduma ya maji kushirikishana uzoefu na mbinu mbalimbali ili kufikia lengo la kufikisha huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza kwa wananchi.

Naye Waziri Suleiman alisema milango kwa Zanzibar ipo wazi kwa watendaji wa Tanzania bara kwenda kuongeza ufanisi mkubwa katika katika sekta maji.



# TARI kugawa mbegu bora za michikichi kwa wakulima

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole imeanzisha kitalu cha miche ya mbegu bora za michikichi wilayani Kyela ili kuwagawia wakulima wa zao hilo katika maeneo yote yanayofaa kulima zao hilo kwenye mwambao wote wa Ziwa Nyasa.

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, aliyasema hayo juzi wakati taasisi hiyo ilipokuwa inatoa elimu kwa maofisa kilimo wa maeneo yote ya Wilaya ya Kyela ambayo yanafaa kwa kilimo cha chikichi.

Alisema walifikia uamuzi huo kwa lengo la kuzalisha chikichi kwa wingi ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa mafuta unaolikabili taifa kwa sasa pamoja na kuwainua wananchi kiuchumi.

"Chanzo kikuu cha tatizo la uhaba wa mafuta nchini ni ukosefu wa malighafi za kutosha kwa ajili ya kuzalisha mafuta, sasa serikali imeamua kumaliza tatizo hilo kwa kuwekeza kwenye kilimo cha mazao yanayosaidia upatikanaji wa malighafi hiyo na ndio sababu nasi tumeamua kuzalisha mbegu za chikichi hapa wilayani Kyela ili kutimiza azma hiyo ya serikali," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema kitalu hicho kitasaidia kupanua kilimo cha zao hilo katika mwambao wa Ziwa Nyasa ambako imebainika kwamba zao hilo linaweza kustawi vizuri.

Alisema miche hiyo itasambazwa kwa wakulima ili wapanue mashamba yao ya chikichi na kwamba baada ya miche hiyo kuanza kutoa matunda, suala la uhaba wa mafuta nchini litabakia kuwa historia.

Mratibu wa Utafiti na Ubunifu wa TARI, Dk. Emmanuel Chilagani, alisema kwa kuanzia wamepanda mbegu 41,000 ambazo endapo zitaota zote watapata miche 41,000 na zisipoota zote wanakusudia kupata miche isiyopungua 27,000.

Alisema miche hiyo wataigawa bure kwa wananchi wa Wilaya ya Kyela na maeneo yote ya mwambao wa Ziwa Nyasa na kwamba elimu wanayoitoa kwa maofisa kilimo itasaidia miche hiyo kwenda kutunzwa ipasavyo.

"Hii miche itatosha kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 220, kwahiyo tunawashauri wakulima wa wilaya hii ya Kyela na maeneo yote ya mwambao wa Ziwa Nyasa wachangamkie fursa hii," alisema Dk. Chilagani.

Naye mtafiti wa michikichi kutoka TARI, Beata Paul, alisema wakulima wengi wa Wilaya ya Kyela wamekuwa wakitumia mbegu za asili ambazo uzalishaji wake hauna tija kubwa kama ilivyo kwa miche ya kisasa na chotara.

Alisema mbegu za kienyeji ambazo wakulima huzitumia huchukua kati ya miaka mitano na saba kuanza kuzaa na mkulima anapata tani 1.6 pekee za mafuta huku za kisasa zinachukua miaka mitatu mpaka mitano kuzaa na mkulima anapata mpaka tani nne za mafuta kwa hekta.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Ezekiel Magehema, alisema wamejipanga kuhakikisha wanawahamasisha wakulima kutumia fursa hiyo kulima zao hilo ili kujiinua kiuchumi.

Alisema tangu mwezi Februari mpaka sasa wataalamu wa kilimo kutoka TARI wamepiga kambi wilayani humo wakitoa elimu na kugawa mbegu za michikichi ili kupanua kilimo hicho.

Alisema kwa sasa wanaendelea kuhamasisha wananchi kutumia mbegu hizo za kisasa na kuachana na za asili ambazo tija yake ni ndogo ikilinganishwa na za kisasa.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (katikati waliokaa), akiwa pamoja na Katibu Tawala wa Mkoa huo, Dk. Angelina Lutambi (kushoto kwake) pamoja na wakuu wa wilaya zote za mkoa huo, baada ya kukutana nao juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Shule zote sasa kuezekwa mabati ya kijani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeagiza shule zote za msingi na sekondari zitakazojengwa mkoani humo kuanzia sasa kuezekwa kwa mabati ya migongo mipana yenye rangi ya kijani ili ziwe na mwonekano tofauti na taasisi zingine.

Pia, imeagiza madirisha ya shule hizo kuwekwa vioo na sakafu yake kuwekwa marumaru ili wanafunzi wasomee katika mazingira ya kuvutia yatakayosaidia kupandisha kiwango cha ufaulu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo juzi alipokuwa anazungumza na wakuu wa wilaya, wakurugenzi na watumishi mbalimbali wa wilaya zote za mkoa huo.

Homera alisema wakuu wa wilaya ndiyo wenye jukumu la kusimamia ujenzi wa miundombinu hiyo na kuwataka kusimamia elimu kikamilifu ili ufaulu wa wanafunzi upande mpaka asilimia 95 kwa ngazi zote za elimu.

"Hili jiji letu linaitwa 'Green City' (Jiji la Kijani), sasa lazima miundombinu yetu iendane na jina letu, kwa hiyo kuanzia sasa shule yoyote itakayojengwa lazima iezekwe kwa mabati ya kijani, hili linawezekana kabisa," alisema Homera.

Mbali na shule mpya zitakazojengwa, pia aliwataka shule yoyote inayofanyiwa ukarabati izingatie matumizi ya vifaa hivyo na kwamba baada ya muda taasisi hizo zitakuwa na mwonekano wa aina moja.

Aliwataka wakuu wa wilaya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha wanashirikiana kujenga vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi watakaojiunga na kidato cha kwanza mwakani ili kuepuka kila mwaka baadhi ya wanafunzi kuchelewa kuanza masomo.

Homera alisema endapo viongozi hao hawatakamilisha miundombinu hiyo, kuna hatari wakazuiwa kwenda likizo mwisho wa mwaka mpaka watakapokamilisha miundombinu hiyo.

Baadhi ya wakuu wa wilaya waliahidi kutekeleza maagizo hayo huku baadhi wakieleza kwamba tayari walishaanza kutekeleza baadhi ya maelekezo hayo hasa la kukabiliana na tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema wilaya yake kwa sasa inaendelea na ujenzi wa shule mpya na kuongeza madarasa kwenye baadhi ya shule ili kukabiliana na tatizo hilo la upungufu wa miundombinu.

Mfune alisema mpaka kufikia mwezi Desemba, mwaka huu, tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa wilayani humo utakuwa umemalizika na wanafunzi wote watakuwa katika mazingira mazuri.

"Tunaendelea na ujenzi wa shule mpya na kuboresha za zamani, sasa kwa yale madarasa ambayo bado hatujaezeka lazima tutaezeka kwa kuzingatia maagizo ya Mkuu wa Mkoa," alisema Mfune.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alisema baada ya kikao hicho anaenda kukaa na wataalamu wa wilaya yake ili wajadiliane namna ya kutekeleza maagizo hayo.

Alisema katika kuboresha sekta ya elimu, wilaya hiyo ilishaanza kusimamia baadhi ya mikakati ikiwamo kuhakikisha wanafunzi wanakula chakula cha mchana wakiwa shuleni.

Mkoa wa Mbeya una jumla ya shule za msingi 756 ambazo kati yake 41 pekee zinamilikiwa na taasisi na watu binafsi na za sekondari 243 ambazo kati yake za binafsi ni 71.

## 'Mazombi' yazua taharuki kwa wakazi wa Itiji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI Mtaa wa Itiji, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wameingiwa na hofu baada ya baadhi yao kuanza kukutana na 'mazombi' nyakati za usiku hali inayowalazimu kufunga shughuli zao mapema wakihofia usalama wao.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara, baadhi ya wananchi hao walisema wamekuwa wakikutana na mauza uza hayo kuanzia saa 2:00 usiku muda ambao wengi wanarudi nyumbani kutoka kwenye shughuli zao.

Mmoja wa wananchi hao, Mwanne Chande alisema tangu matatizo hayo yalianza mwanzoni mwa mwezi huu na kwamba wamekuwa wakiogopa hata kwenda madukani kununua mahitaji nyakati za usiku kuepuka kukutana na madudu hayo.

"Ni kweli serikali haiamini uchawi, lakini kwa kinachoendelea kwenye maeneo yetu ni uchawi, juzi nilisikia mbwa zinabweka nje nilipoenda kuchungulia sikuona mbwa na badala yake niliona vitu vyeupe na vilipotea kama upepo," alidai Mwanne.

Alisema baada ya siku mbili alitoka dukani na kukutana na mtu mrefu wa ajabu na ndipo akaamua kufikisha taarifa za uwapo wa maajabu hayo kwa mwenyekiti wa mtaa.

Alisema wakazi wa eneo hilo kwa sasa wanaomba mtu aliyefuga mazombi hayo ayaondoe ili waendelee na shughuli zao kwa amani kwa madai kuwa hata kama hayadhuru, lakini watu wanaweza wakaumia kwa kuyakimbia.

Mwenyekiti wa mtaa huo, Augustino Kansapa, alikiri kuwapo kwa tatizo la mazombi hayo na waliamua kuitisha mkutano ili wawasikilize wananchi waliokutana nayo na jinsi ya kukabili tatizo hilo.

Alisema baadhi ya wananchi walikuwa wanawatuhumu baadhi ya wenzao kuwa ndio wanaomiliki mazombi hayo hali iliyokuwa inatishia amani.

"Sisi kama serikali tumeamua kuitisha mkutano ili tutoane hofu na kwasababu baadhi ya wenzetu wanatuhumiwa tumeona ni vyema tutoe elimu maana hili jambo linaweza likasababisha mauaji kwenye eneo letu," alisema Kansapa.

Aliwaomba baadhi ya wazee wa mtaa huo kukaa na watu waliokuwa wanatuhumiwa ili wasaidie kumaliza tatizo hilo ambalo limezua hofu kwenye eneo hilo.



# Matukio 66 udhalilishaji kijinsia yaripotiwa Mei

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MATUKIO 66 ya udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa kwa mwezi wa Mei, mwaka huu, Zanzibar huku Wilaya ya Magharibi A Unguja ikiongoza kwa kuwa na matukio 15.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Kitengo cha Makosa ya Jinai, Madai na Jinsia katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Mwanajuma Ali Suleiman, alisema matukio hayo 43 ni ubakaji, saba ulawiti, tisa shambulio la aibu na saba kutorosha wasichana na wanawake.

Alisema waathirika wa matukio hayo ni watoto ambao ni asilimia 87.9 na wanawake ni asilimia 12.1.

Mwanajuma alisema mlinganisho wa matukio hayo kwa mwezi umepungua kwa asilimia 38.9 kutoka matukio 108 kwa mwezi wa Aprili, mwaka huu.

Pia alisema matukio 62 yako chini ya upelelezi wa polisi na matukio manne yako katika hatua zingine, mawili ya mahakamani na matukio mawili katika ofisi ya mkurugenzi wa mashtaka.

Naye Mrakibu Msaidizi wa Polisi Zanzibar, Ramadhan Jimid Haji, alisema kesi hizo zina changamoto zake katika kufanya upelelezi.

Alisema baadhi ya watu katika jamii hawako tayari kutoa ushahidi wa kesi hizo ili polisi kukamilisha uchunguzi wake.

Kutokana na changamoto hiyo, aliitaka jamii kutoa ushirikiano katika kutoa ushahidi ili watuhumiwa wafikishwe katika vyombo vya sheria.



Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), Joyce Shebe (katikati), akikagua ujenzi wa kituo cha jinsia cha chama hicho, huko Tunguu, Wilaya ya Kati Unguja juzi. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Uhasibu wa TAMWA Zanzibar, Mohamed Khalid. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# TAMWA yaeleza manufaa kituo cha jinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Joyce Shebe, amesema uanzishwaji wa kituo cha jinsia cha chama hicho Zanzibar utaleta tija kubwa kwa manufaa ya jamii na serikali.

Aliyasema hayo juzi alipotembelea ujenzi wa jengo hilo, Tunguu Wilaya ya Kati Unguja na kueleza kuwa wanachama wana kila sababu ya kujivunia uanzwaji wa kituo hicho.

Shebe alisema kwa miaka mingi tangu kuanzishwa kwa chama hicho hakujawahi kufanyika uwekezaji mkubwa wa aina hiyo na kwamba kufanyika kwake kuna nguvu kubwa ambayo inaendelea kuwekezwa na inahitaji kuendelezwa. Kwa mujibu wa Shebe, katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, wananchi wanakabiliwa na ukosefu wa elimu ya jinsia kiasi kwamba miongoni mwao hujikuta wakingia kwenye matatizo.

Alisema kukamilika kwa ujenzi huo kutaibua fursa kwa wananchi wa Zanzibar kujifunza elimu ya jinsia ambayo itasambaa na kusaidia wengine hatimaye kuwa na jamii yenye mabadiliko na kutambua umuhimu wa usawa wa kijinsia. Mwenyekiti huyo alitoa wito kwa jamii na taasisi mbalimbali za binafsi na serikali kujitokeza kuunga mkono ujenzi huo.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa jengo hilo, Shifaa Said Hassan, alisema ujenzi huo ulianza Januari, mwaka huu, na hadi sasa Sh. milioni 358 zimetumika na asilimia 99 ya gharama zimechangiwa na TAMWA upande wa Zanzibar.

Alisema ili jengo hilo likamilike kwa ghorofa ya kwanza na kuanza kutumika, zinahitajika Sh. 570,297,000, hivyo kuwaomba wahisani kusaidia kwa kuwa elimu ya jinsia ni muhimu kwa kila mwananchi.

# Ahimiza ushirikiano wa elimu mjumuisho

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Uendeshaji na Utumishi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Omar Ali Omar, amesema ushirikiano unahitajika katika kuhakikisha lengo la serikali la kuanzishwa elimu mjumuisho linafikiwa.

Akifungua mkutano wa kwanza wa Kamati ya Uongozi ya Elimu Mjumuisho ambao ulikwenda sambamba na utambulisho wa mradi wa elimu mjumuisho jana, Omar alisema lengo la serikali ni kutaka watoto wote wapate elimu itakayowanufaisha kwa maisha yao ya baadaye.

Alisema serikali inatambua kwamba mifumo yao kuhusu elimu mjumuisho haiko sawa lakini waangalie walimu ambao wamepatiwa mafunzo juu ya kuwafundisha watoto hao kuwapeleka sehemu zenye mahitaji.

Hata hivyo alisema katika kufikia malengo hayo mbali na kuwapo vikwazo mbalimbali, walimu wanatakiwa kuwa na utayari juu ya jambo hilo ili watoto ambao ni wenye ulemavu wapate elimu sawa na wasio na ulemavu.

"Utayari ni jambo muhimu katika suala hili kwani tunajua kwamba watoto wetu ambao wanapata elimu wana mahitaji mbalimbali, hivyo utayari ni jambo la kuzingatia katika ufundishaji hasa kwa vile tunajua wengi wetu kwamba kuwa mwalimu ni kazi ya kujitolea," alisema.

Wakichangia katika kikao hicho, wajumbe walisema bado kuna vikwazo vingi katika elimu mjumuisho ambavyo kutatuliwa kwake kunahitaji nguvu za pamoja.

Walisema watoto wenye ulemavu wana matatizo mbalimbali na hata wale wasiokuwa na ulemavu ambavyo ili kuvitatua kwake ni lazima kuzitambua mapema.

Aidha, walisema elimu mjumuisho inapaswa itambulishwe kwa watu wote na si kwa watu maalumu ili kila mmoja aifahamu.

Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Jumuiya ya Makuzi ya Awali ya Mtoto (MECPz), Mohammed Dau, alisema lengo la mradi huo ni kutaka kuona elimu mjumuisho inatolewa katika Shule zote Unguja na Pemba.

"Elimu mjumuisho inagusa watoto wote awe mwenye ulemavu au asiye na ulemavu ili kila mmoja aweze kupata kusoma kwa mafanikio, kuwepo kwa matabaka tutakuwa tunaelekea kule ambako tulikotoka," alisema Dau.

Mradi huo wa miaka mitano unafanyika katika wilaya tatu za Mjini na Kusini kwa Unguja na Chakechake kwa Pemba unafadhiliwa na Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu ya Norway na kusimamiwa na MECPz.

## SADC kupeleka wanajeshi mpaka Msumbiji, Tanzania

**Maputo,** MSUMBIJI

MATAIFA ya Jumuiya ya Kusini mwa Afrika (SADC), yamekubaliana kutuma wanajeshi Msumbiji kukabiliana na wanajihadi katika mkoa wa Cabo Delgado ambao unashuhudia matatizo ya kiusalama, Kaskazini mwa nchi hiyo.

Hata hivyo, haijafahamika kwa kina kuhusu kikosi hicho na muda ambao kitatumia kukabiliana na manajihadi hao, mapema mwaka huu, iliripotiwa kuwa SADC inatarajiwa kutuma wanajeshi 3,000.

Mwenyeji wa mkutano huo, Rais Filipe Nyusi wa Msumbiji ambaye ni mwenyekiti wa sasa wa SADC aliitisha mkutano huo, ili kuomba usaidizi wa marais wenzake kuhusu kitisho cha wanamgambo wanaohusishwa na kundi linalojiita Islamic State IS, ambao wanaendesha mashambulizi katika jimbo la Capo Delgado, Kaskazini mwa Msumbiji.

Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya SADC, Stragomena Pax, alisema marais hao wamekubaliana kupeleka kikosi cha pamoja cha jumuiya hiyo Msumbiji, ili kuimarisha usalama wa eneo hilo, huku wakitoa wito wa kupewa msaada wa kimataifa katika mapambano yake dhidi ya ugaidi.

Wapiganaji wa kigaidi wameshutumiwa kwa kufanya mauaji ya kikatili tangu mwaka 2017 kwa kufanya uvamizi wa vijiji na miji maeneo ya mpaka kati ya Msumbiji na Tanzania.

**RFI**

## Serikali mpito Libya kuitisha uchaguzi

**Berlin,** UJERUMANI

SERIKALI ya mpito ya Libya imesisitiza azma yake ya kuitisha uchaguzi Desemba 24, mwaka huu, wakati wa mkutano wa Jumatano mjini Berlin, Ujerumani ambayo ni mwenyeji wa kikao hicho, ikisema kuwa itaendelea kutoa shinikizo hadi vikosi vyote vya kigeni viondolewe.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Associated Press, Ujerumani pamoja na Umoja wa Mataifa (UN), waliyaleta pamoja mataifa 17 kwenye mkutano huo, wakati serikali na maofisa wa serikali ya mpito ya Libya wakiandamana na mawaziri wa kigeni wa Misri, Uturuki, Tunisia, Algeria, Ufaransa na Italy.

Miongoni mwa maofisa wengine wa ngazi za juu waliohudhuria ni Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken na maofisa kutoka Russia na Umoja wa falme za Kiarabu.

Wakati wa kikao hicho, Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Heiko Maas, alisema wameingia ukurasa mpya kwa kuwa sasa hawazungumzii kuhusu Libya bali sasa taifa hilo ni miongoni mwa washiriki. Kikao hicho kimefuatia kile cha mwaka 2020, viongozi walikubaliana kutoyauzia silaha makundi yanayozozana nchini Libya pamoja na kuyashinikiza kusitisha kabisa mapigano.

**VOA**

# 10 familia moja wafa wakinywa mitishamba

**Kwara,** NIGERIA

POLISI katika Jimbo la Kwara katikati ya Nigeria wanasema watu 10 wa familia moja, wamekufa baada ya kunywa mchanganyiko wa mitishamba kama dawa za jadi.

Kisa hicho kilitokea katika kijiji cha Biogberu baada ya wanaume wawili kumfuata mwanamke mmoja, aliyekuwa na ugonjwa wa miguu na kumpa mchanganyiko wa mitishamba kama tiba.

Inasemekana walitoa sharti kwamba watu wote wa familia yake lazima watumie mchanganyiko huo ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa kati yao.

Katika taarifa iliyotolewa juzi na Msemaji wa Polisi katika Jimbo la Kwara, Okasanmi Ajayi, wale wote waliokunywa dawa hiyo ya kienyeji baadaye walifariki.

Aliiambia BBC kwamba mtu wa mwisho kati ya jamaa hao 10 wa familia moja alifariki, akiwamo mgonjwa wa kwanza.

Ajayi aliongeza kuwa mwathiriwa mdogo alikuwa mtoto wa miaka miwili na mtu mzima wa miaka 40. Polisi walisema washukiwa wawili walikamatwa na uchunguzi unaendelea. Haijabainika ikiwa ni wauguzi wa kienyeji kutoka jamii ya eneo hilo.Baadhi ya Wanigeria hasa kutoka maeneo ya mashambani, wanategemea tiba za kienyeji kutokana na ukosefu wa kujua kusoma na kuandika, imani ya kitamaduni na umaskini. Mfumo wa afya wa nchi hiyo pia unakabiliwa na changamoto kadhaa. **BBC**



Uokoaji ukiendelea baada ya jengo lenye makazi ya watu, kuporomoka jana, jimbo la Miami-Dade, jijini Florida, nchini Marekani na kuua mtu mmoja. Haikufahamika mara moja idadi ya watu waliokuwamo ndani wakati jengo hilo likiporomoka. **PICHA: BBC**

# Museveni ateua Mkuu wa Majeshi

**Kampala,** UGANDA

RAIS wa Uganda Yoweri Museveni, amemteua Jenerali Wilson Mbadi kuwa mkuu mpya majeshi wa nchi hiyo (CDF).

Kabla ya uteuzi huo, Mbadi alikuwa msaidizi wa Mkuu wa Majeshi na mlinzi binafsi wa Rais Museveni aliyedumu kwa muda mrefu.

Jenerali Peter Elwelu aliyekuwa mkuu wa majeshi ya ardhini atakuwa mkuu wa majeshi msaidizi. Jenerali Elwelu anakumbukwa kwa kuongoza jeshi kuvamia makazi ya mfalme wa Rwenzururu, Magharibi mwa Uganda mwaka 2016, ambapo kwa mujibu wa taarifa rasmi zaidi ya watu 80 walidaiwa kufariki dunia.

Kwa uteuzi huo sasa anakuwa pia mwakilishi wa Jeshi bungeni, kufuatia mabadiliko hayo, mtoto wa Rais Museveni, Jenerali Muhoozi Kainerugaba sasa atakuwa anaongoza vikosi vya ardhini.

Muhoozi alikuwa anaongoza vikosi maalumu vya ulinzi binafsi wa Rais.

Mabadiliko hayo yanafuatia Jenerali David Muhoozi, ambaye alikuwa mkuu wa majeshi, kuteuliwa hivi karibuni kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, kuchukua nafasi ya Obiga Kania.

Katika siku za hivi karibuni, Rais Museveni alikuwa akifanya mabadiliko ya mara kwa mara kwenye jeshi la nchi hiyo, maofisa vijana wa jeshi wamekuwa wakichukua nafasi za juu zilizokuwa chini ya maveterani walipigana vita katika miaka ya 1980.

**BBC**



# ENGLAND, UJERUMANI USO KWA USO 16-BORA EURO

**LONDON, England**

BAADA ya mechi za mwisho za makundi, droo ya hatua ya mtoano wa timu 16 kwenye michuano ya Euro 2020, imekamilika huku England ikipangwa kukutana na Ujerumani kwenye Uwanja wa Wembley, Jumanne ya Juni 29, mwaka huu.

Kocha wa England, Gareth Southgate, atakuwa na kumbukumbu mbaya kuelekea mchezo huo, kwani alikosa penalti dhidi ya Ujerumani kwenye nusu fainali ya Euro 1996 katika dimba la Wembley na 'Simba Watatu' hao walitolewa kwa mikwaju ya matuta 6-5.

Miamba hiyo ikakutana tena kwenye Euro 2000 hatua ya makundi, lakini ilishinda 1-0 shukrani kwa bao la Alan Shearer na timu zote zilitinga hatua ya mtoano.

Ujerumani ilionekana kama isingefuzu kwenye hatua hiyo katika michuano hii kutoka Kundi F kabla ya kupata sare ya mabao 2-2 na Hungary, Jumatano.

Sare ya mabao 2-2 kati ya Ureno na Ufaransa kilikifanya kikosi kinachoongozwa na Cristiano Ronaldo kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo na sasa kitakutana na Ubelgiji Jumapili mjini Seville nchini Hispania.

Ratiba yote ya Euro 2020 hatua ya 16-bora

Jumamosi, Juni 26: Wales vs Denmark (Uwanja Johan Cruyff Arena, Amsterdam), Italia vs Austria (Uwanja Wembley, London).

Jumapili, Juni 27: Uholanzi vs Jamhuri ya Czech (Uwanja Puskas Arena, Budapest), Ubelgiji vs Ureno (Uwanja La Cartuja, Seville).

Jumatatu, Juni 28: Croatia vs Hispania (Uwanja Parken, Copenhagen), Ufaransa vs Uswisi (Uwanja National Arena, Bucharest).

Jumanne, Juni 29: England vs Ujerumani (Uwanja Wembley); Sweden vs Ukraine (Uwanja, Hampden Park).

## MESSI AKUBALI KUSAINI MKATABA MPYA BARCA



**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi atasaini kuongeza mkataba mpya na Barcelona utakaomuweka hapo Camp Nou hadi mwaka 2023, kwa mujibu wa mwandishi wa Sky Sport Italia, Fabrizio Romano.

Mkataba wake wa sasa wa Messi na Barcelona na mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, unamalizika mwishoni mwa mwezi huu.

Na kwa muda mrefu nyota huyo wa kimataifa wa Argentina amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa miamba hao wa Catalunya.

Lakini sasa, Romano ameripoti kuwa Messi atasaini mkataba wake huo na Barca kwa muda wa miaka miwili.

Messi alikuwa akihusishwa zaidi na klabu za Manchester City na Paris Saint-Germain.

Na sasa Messi amekubali kusaini mkataba mpya wa kuendelea kucheza hapo Barcelona kwa misimu miwili zaidi.

Ripoti hiyo inasema kwamba, Messi amefikia makubaliano na Rais wa Barcelona, Joan Laporta na amekubali kuongeza mkataba wake.

Messi kwa sasa yupo na Argentina kwenye majukumu ya kimataifa kwenye michuano ya Copa America 2020.

## RODRIGUEZ AHUSISHWA KUTUA ATLETICO MADRID

**LONDON, England**

HATIMA ya James Rodriguez inaonekana kama inataka kutawala kwa mara nyingine vichwa vya habari kupitia dirisha la usajili la kipindi hiki cha majira ya joto.

Kuendelea kwake kusalia Everton kunaonekana kuwa kwenye shaka kubwa baada ya kuondoka kwa aliyekua Kocha Mkuu, Carlo Ancelotti aliyetimkia Real Madrid kwa mara nyingine.

Kwa mujibu wa Daily Mail, wakala wa nyota huyo wa kimataifa wa Colombia, Jorge Mendes, Rodriguez amepata ofa kutoka AC Milan, Napoli na Atletico Madrid.

Mwaka 2019, nyota huyo alikaribia kutua Atletico kabla ya dili hili kushindikana dakika za mwisho.

Hatua inayowezekana inaonekana kurudi tena, ingawa vizuizi kadhaa vinahitaji kuondoshwa ili mpango kufanyika, kama Atletico itakuwa tayari kulipa mahitaji makubwa ya mshahara kwa mchezaji anayekaribia miaka 30.




# ARSENAL YATOA OFA KWA WHITE

**LONDON, England**

ARSENAL imeripotiwa kuweka wazi kuwa iko tayari kutumia kiasi cha pauni milioni 50 kumsajili beki wa kati wa Brighton & Hove Albion, Ben White wakati wa usajili wa majira haya ya joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, alikuwa na msimu wa kuvutia wa 2020-21 na alipewa nafasi katika kikosi cha England kwenye mashindano ya Ulaya .



Chelsea, Liverpool na Manchester United zote zimetajwa kuvutiwa na beki huyo, ambaye bado amebakiza miaka mitatu kukamilisha mkataba wake na kikosi cha kocha Graham Potter.


Hata hivyo, ripoti ya hivi karibuni ilidai kwamba Arsenal pia walikuwa fiti kunasa saini yake, na kwa mujibu wa The Athletic, 'Washikabunduki' hao sasa wanaandaa ofa ya huduma yake.

Ripoti hiyo inadai kwamba klabu hiyo ya London Kaskazini inaweza kufanya makubaliano kwa pauni milioni 40, lakini kikosi hicho cha kocha Mikel Arteta kitakuwa tayari kufikia hadi pauni milioni 50.

# PSG KUMRUDISHA TENA LUIZ PARIS

**PARIS, Ufaransa**

TETESI mbalimbali za hivi karibuni zimemhusisha beki wa zamani wa Benfica na Chelsea, David Luiz, kurejea katika klabu ya Paris Saint Germain ambayo aliwahi kuitumikia kabla.



Inaaminika Rais wa klabu hiyo ya jijini Paris, Nasser Al-Khelafi ni shabiki mkubwa wa raia huyo wa Brazil, lakini kocha, Mauricio Pochettino ana mashaka juu ya uhamisho huo.

Kwa mujibu wa The Sun, PSG wanapanga kumrejesha beki huyo baada ya mkataba wake na klabu ya Arsenal kumalizika katika majira haya ya joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ataondoka kama mchezaji huru msimu huu wa majira ya joto, na anaweza kurudi kwa miamba hiyo ya Ligue 1, ambapo alicheza kati ya mwaka 2014 na 2016.

Rais Al-Khelafi ameripotiwa kuwa yupo tayari kutoa kiasi cha fedha kwa ajili ya kumsajili Luiz.

Kikwazo kinaweza kuwa kocha Pochettino ambaye ameonyesha kutokuwa na nia ya kumhitaji Luiz.



# MILAN

## WAFIKIA PAZURI USAJILI WA GIROUD

**MILAN, Italia**

KLABU ya AC Milan, imeripotiwa kwamba imefikia makubaliano ya kumsajili, Olivier Giroud kwa mkataba wa miaka miwili kutoka Chelsea.

Licha ya Giroud kusaini mkataba wa mwaka mmoja kuendelea kucheza pale Stamford Bridge, bado hatma yake klabuni hapo kwa msimu ujao haijulikani.

Milan wamemaliza msimu wa Serie A wakiwa nyuma ya mahasimu wao wa jiji moja, Inter Milan katika msimamo wa ligi hiyo na sasa wanajiandaa kukisuka kikosi chao kwa ajili ya msimu ujao.

Sambamba na Giroud, Milan wanamuwinda Hakim Ziyech ambaye wanamuona kama mbadala sahihi wa Hakan Calhanoglu ambaye ametimkia Inter kama mchezaji huru.

Milan pia wanampango wa kurudi kumchukua, Tiemoue Bakayoko ambaye aliitumikia klabu hiyo kwa mkopo msimu uliopita.

Endapo Milan watafanikiwa katika hili, watakuwa wamechukua jumla ya wachezaji wanne wa Chelsea kwa misimu miwili ikiwa ni pamoja na Fikayo Tomori ambaye wamekamilisha usajili wake wa kudumu.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO AFIKIA REKODI YA MABAO MENGI KIMATAIFA

**●●●Aungana na Ali Daei kuwa mfungaji bora wa wakati wote, pia avunja ya Michel Platini Euro...**

**BUDAPEST, Hungary**

NYOTA wa Ureno, Cristiano Ronaldo, ameifikia rekodi ya muda mrefu iliyowekwa na Ali Daei wa Iran ya kufunga mabao mengi zaidi kwenye mechi za kimataifa 109, juzi.

Ronaldo ambaye ni nahodha wa Ureno, aliifikia rekodi hiyo baada ya kufunga mabao mawili wakati Ureno ikitoka sare na Ufaransa kwenye mchezo wa Euro 2020.

Nyota huyo wa Juventus amefanya uwapo wake uwe muhimu sana kwenye mashindano ya msimu huu wa majira ya joto, bao lake moja alilifunga kwa mkwaju wa penalti dhidi ya Ufaransa wakati wa mchezo wao wa mwisho wa Kundi F na kufanikiwa kufuzu hatua ya mtoano wa timu 16-bora.

Kwa kufanya hivyo, Ronaldo alifunga bao la kimataifa la 109 Jumatano jioni, akilingana na rekodi iliyowekwa na mshambuliaji huyo wa zamani wa Iran, Daei, ambaye alistaafu soka la kimataifa mwaka 2006.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, pia alimzidi Miroslav Klose kama mchezaji aliyefunga mabao mengi kwenye Euro na Kombe la Dunia wakiwa pamoja (20) na alivunja rekodi ya mabao ya mashindano na Ulaya ya Michel Platini wakati wa ushindi wao dhidi ya Hungary mapema kwenye mashindano hayo.

Ronaldo sasa amefunga jumla ya mabao matano wakati wa michezo mitatu ya Ureno katika Kundi F, na mabingwa watetezi hao sasa watakutana na Ubelgiji katika hatua ya 16-bora Juni 27, mwaka huu.

Hatma ya Klabu gani atakuwapo msimu ujao bado inaendelea kuwa sintofahamu kwa mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, na Juve inadaiwa wana orodha ya watu saba wanaoweza kuchukua nafasi ikiwa ataondoka pale Turin.

## KWA UFUPI

### MESSI BADO KUAMUA
MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, bado hajafanya uamuzi iwapo atasalia Barcelona au la, akiwa amebaki na wiki moja kumaliza mkataba wake na klabu hiyo ya Hispania. ***(Marca)***

### PSG YAMUWANIA RAMOS
KLABU ya Paris St-Germain, imewasiliana na Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 35, ambaye mkataba wake na Real Madrid unamalizika mwisho wa mwezi huu. ***(Goal)***

### SPURS WAMTAKA NUNO
KLABU ya Tottenham Hotspur inapanga kufanya mazungumzo na kocha wa zamani wa Wolves, Nuno Espirito Santo kuhusu mpango wa kuchukua nafasi ya ukocha, baada ya awali kumuacha nje ya kinyang'anyiro Mreno huyo mwenye miaka 47. ***(Football Insider)***

### MAN CITY KUSUBIRI STRAIKA
MANCHESTER City iko tayari kusubiri kwa mwaka mmoja zaidi kumpata mshambuliaji mwingine iwapo juhudi zao za kumsajili Harry Kane mwenye umri wa miaka 27 kutoka Tottenham msimu huu wa majira ya joto zitagonga mwamba. ***(ESPN)***

### RODRIGUEZ KUSEPA EVERTON
WAWAKILISHI wa straika wa Everton, James Rodriguez, wamemnadi mchezaji huyo kwa klabu kubwa za Ulaya Real Madrid, Atletico Madrid, AC Milan na Napoli baada ya nyota huyo wa kimataifa wa Colombia mwenye umri wa miaka 29, kuonyesha yuko tayari kuondoka pale Goodison Park. ***(Mail)***

### HAKIMI ANUKIA PSG
PSG pia wameafikiana na Inter Milan kumsaijili winga wa Morocco, Achraf Hakimi mwenye umri wa miaka 22 kutoka klabu hiyo ya Serie A kwa ofa ya Euro milioni 59.8, ikijumuisha marupurupu ya ziada. ***(ESPN)***

### ARSENAL KUMFUNGA ROWE
ARSENAL wanaamini watafanikiwa kumshawishi kiungo wa kati wa England, Emile Smith Rowe mwenye umri wa miaka 20, kumpa mkataba mpya licha ya Aston Villa kuonyesha nia ya kutaka kumnunua. ***(Football London)***

### KLOPP AMTAKA MCGINN
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, anavutiwa na kiungo wa kati wa Aston Villa na Scotland, John McGinn, lakini itahitaji kati ya pauni milioni 45 hadi 50 kumshawishi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kundoka pale Villa Park. ***(The Athletic)***

### TUANZEBE KUONDOKA UNITED
NYOTA wa Manchester United, Axel Tuanzebe mwenye umri wa miaka 23, anatarajiwa kuondoka klabu hapo kwa mkopo msimu huu wa majira ya joto. ***(Manchester Evening News)***

### BERTRAND KUJIUNGA NA LEICESTER
RYAN Bertrand mwenye umri wa miaka 31, anayecheza safu ya ulinzi anajiandaa kujiunga na Leicester City kwa uhamisho wa bure mwanzo mwa Julai hadi mwisho wa mkataba wake na Southampton. ***(Goal)***

### GILMOUR KUTUA CHELSEA
KLABU ya Wolves inawania kumsajili nyota wa kimataifa wa Scotland, Billy Gilmour mwenye umri wa miaka 20, kama mchezaji huru kutoka Chelsea. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

# WAGOMBEA ZFF WAJINADI NA SERA UDHAMINI LIGI KUU

**Sabato Kasika na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI ikiwa imebaki siku moja tu ya kesho kabla ya uchaguzi wa nafasi ya Urais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kufanyika Jumapili wiki hii, wagombea wa nafasi hiyo wamezidi kujinadi kwa sera zao kwa kushawishi wajumbe kuwapigia kura.

Uchaguzi huo unafanyika kutokana na kujiuzulu kwa aliyekuwa Rais wa ZFF, Seif Kombo Pandu, mapema Februari mwaka huu na jumla ya wagombea watano wamepitishwa kuwania nafasi hiyo ambao ni Abdulatif Ali Yasini, Suleiman Shaban Suleiman, Haji Shehe Hamad, Suleiman Mahmoud Jabir na Abdulkadir Mohamed Abdulkadir "Tash".

Akimwaga sera zake kuelekea uchaguzi huo, mmoja wa wagombea, Jabir alisema, iwapo atachaguliwa atahakikisha kunakuwa na mashindano ya Super Cup yatakayoshirikisha timu za Zanzibar na Tanzania Bara.

Jabir aliyasema hayo katika taarifa yake ya kampeni aliyoitoa kwa vyombo vya habari juzi, kuelezea sera zake iwapo atachaguliwa kuongoza chombo hicho cha soka visiwani humo katika uchaguzi utakaofanyika Jumapili.

Alisema kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), serikali zote mbili na wadhamini, ataanzisha mashindano yatakayoshirikisha timu za Zanzibar na Tanzania Bara ya Super Cup.

"Huko nyuma yalikuwapo mashindano ya Ligi ya Muungano, yaliyoshirikisha timu tatu kutoka Bara na nyingine Zanzibar na bingwa wake aliiwakilisha Tanzania katika Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema katika taarifa hiyo.

Mgombea mwingine wa nafasi hiyo, Yasini alisema endapo wajumbe watamchagua kuwa Rais wa ZFF, atahakikisha anashughulikia suala la udhamini katika Ligi Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema atasimamia kuwapo kwa sera nzuri ya soka itakayowezesha kupatikana wadhamini wa Ligi Kuu Zanzibar itakayosaidia mpira kuchezwa bila changamoto ya udhamini.

Alisema jambo lingine ni kuhakikisha anashughulikia migogoro ya uongozi katika baadhi ya vyama vya shirikisho hilo ili kudumisha ushirikiano kati yao huku pia akiendeleza mashirikiano baina ya ZFF na TFF.

"Hakuna njia ambayo sisi itaepukika kwa kutokuwa na ushirikiano na TFF maana mambo mengi ya mashirikisho ya nje moja kwa moja yanapitia kwao, hivyo lazima tuwe na ushirikiano mzuri ili tuweze kunufaika sote," alisema.

MAGONGO...



Wanafunzi wa Al-Madrasa Tus Saifen ya Upanga jijini Dar es Salaam (jezi za njano na kijani), wakiwania mpira na wanafunzi wa Sekondari ya Buza jana katika mchezo wa mpira wa magongo kwenye Michuano ya Likizo Cup inayofanyika katika viwanja vya Jakaya Kikwete na kudhaminiwa na T.H.A Tanzania Hockey Association. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Azam yamnasa Jesi, yajichimbia Zambia

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC, umesema uko katika hatua nzuri za kukamilisha mchakato wa usajili wa kiungo kutoka Al Hilal ya Sudan, Mzimbabwe Last Jesi, ambaye atatia saini mkataba wa miaka miwili kuwatumikia wakali hao wa Chamazi, Dar es Salaam kuanzia msimu ujao wa 2021/22.

Mbali na kiungo huyo, taarifa zimeeleza kuwa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat', yuko nchini Zambia kwa mazungumzo na nyota wengine akiwamo Collins Shikombe na Benson Sakala, ambao pia ni wachezaji wa timu ya Taifa ya Zambia.

Popat ameliambia gazeti hili kwa simu akiwa nchini Zambia, kuwa wako katika hatua za mwisho kumalizana na Jesi, ambaye tayari yuko Dar es Salaam kwa ajili ya kukamilisha dili hilo.

Alisema Jesi yuko katika mipango yao, na kuhusu viungo wawili ambao ni Shikombe na Sakala, Popat alisema hawapo katika mipango yao kwa sababu si mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Mzambia George Lwandamina.

"Kweli Jesi yuko katika mipango yetu ya usajili na mambo yakienda vizuri atakuwa miongoni mwa wachezaji wetu kwa msimu ujao, kuhusu Shikombe na Sakala si kweli na wala hawako katika mipango ya usajili wetu.

"Jesi yuko Dar es Salaam, Tanzania na anafanya mazoezi hapo Chamazi akisubiri kukamilisha taratibu zetu za usajili, mbali na huyo tunaendelea vizuri na mchakato wa kusajili kulingana na mapendekezo ya benchi la ufundi ya timu yetu," alisema Popat.

Alisema mbali na ujio wa kiungo huyo pia wako katika mchakato wa kutafuta nyota wengine wakigeni kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na michuano ya kimataifa wakati huu tayari wakiwa na uhakika wa kushiriki kwa msimu ujao.

## Gwambina FC hali bado tete Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwangwo**

USHINDI wa mabao 2-0 ilioupata Gwambina FC kwenye uwanja wake wa nyumbani dhidi ya Dodoma Jiji, bado haujaifanya timu hiyo kuondoka kwenye mstari wa hatari wa kuepuka kushuka daraja.

Gwambina imefikisha alama 34 na ipo kwenye nafasi ya 16, huku imebakiza michezo miwili tu kabla ya kumaliza mechi zake 36 za ligi hiyo msimu huu.

"Mechi ilikuwa ngumu, lakini sisi tulijiandaa kwa hilo na tulitarajia kupata ushindi. Mara nyingi ukiangalia hata kwenye rekodi zetu msimu huu, mechi za nyumbani sisi zinakuwa ngumu sana kupata matokeo, lakini kwa hili tulijipanga," alisema Kocha Msaidizi wa timu ya Gwambina FC, Hassan Salum.

Alisema wanatarajia mechi zitasimama kupisha Kombe la FA, hivyo wao wataendelea na mzoezi makali kwa ajili ya mechi mbili zilizobaki, kuhakikisha wanashinda ili kuepuka kushuka daraja.

Naye Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Mbwana Makata, alisema makosa waliyoyafanya mwanzoni ndiyo yamewagharimu.

"Kweli tumepoteza dakika za mwanzoni tumefanya makosa, tukapigwa mabao mawili. Kipindi cha pili tulibadilika, lakini tatizo lilikuwa ni kuzitumia nafasi zilizopatikana," alisema kipa huyo wa zamani wa Tukuyu Stars na Yanga wakati huu timu yake ikiwa na pointi 42.

## Matu na mkakati JKU kutisha Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa timu ya JKU, Omar Khamis "Matu", amesema msimu huu wa ligi ambao bado Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), halijatangaza utaanza rasmi mwezi gani, amekusudia kuwa na kikosi kizuri kitakachotoa ushindani ikilinganishwa na msimu uliopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema JKU msimu huu itakuwa na wachezaji wazuri wenye kuhimili mikikimikiki ya ligi hiyo ambayo imeonyesha kuwa na ushindani mkubwa msimu huu.

Alisema kuwa miongoni mwa mambo anayokusudia kuyafanya ni pamoja na kuwa na mpango mzuri wa mazoezi hususan kwa washambuliaji wake ili waweze kuwa na maamuzi ya haraka pale wanapokaribia lango la wapinzani.

"Tunakusudia kuwa na mazoezi ya mapema pale tu ZFF kupitia kamati yake ya mashindano pamoja na Bodi ya Ligi itakapotoa kalenda yake ya ligi kwa msimu mpya wa 2021/22, ili tufanye vizuri lazima tuwe na maandalizi ya mapema," alisema.

# Michezo

Ijumaa Juni 25, 2021

Nipashe




## RONALDO AFIKIA REKODI YA MABAO MENGI KIMATAIFA

HABARI UK 22

## MCHOMO...



Kipa wa Ufaransa, Hugo Lloris, akiokoa 'mchomo' wa mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo (kushoto), wakati timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2 kwenye mechi ya Kundi F ya michuano ya Euro 2020 iliyopigwa Uwanja wa Ferenc Puskas jijini Budapest, Hungary juzi. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA SAIZI YETU - BIASHARA

## ●●●Makocha kila mmoja atamba kushinda leo na kutinga fainali, lakini rekodi zaibeba...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga ikieleza kwamba inataka kwenda michuano ya kimataifa msimu ujao kwa nguvu zake yenyewe na si kwa kubebwa na nafasi ambazo Simba imezitengeneza, wapinzani wao kwenye nusu fainali ya Kombe la FA, Biashara United wamesema "Yanga ni saizi yetu tutawachapa".

Msimu ujao Tanzania itaingiza timu nne kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), kutokana na mafanikio ya Simba kwenye Ligi ya Mabingwa baada ya kufika robo fainali na kuiwezesha nchi kufikisha pointi 27.5, hivyo kuwa miongoni mwa mataifa 12 yatakayoingiza timu mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho.

Yanga itakuwa ikijaribu kuingia hatua ya fainali kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2015/16, itakapocheza dhidi ya Biashara United leo katika nusu fainali ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora, michuano ambayo bingwa hupata nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga, ambayo iliingia kwenye hatua hiyo kwa kuichapa Mwadui FC mabao 2-0, itakuwa na kazi kubwa ya kufanya kama msimu wa 2015/16 ilipofanikiwa kutinga fainali kabla ya kutwaa kombe hilo kwa kuifunga Azam FC mabao 3-1.

Itaikabili, Biashara United, ambayo imefika hatua hiyo kwa mara ya kwanza, ingawa kwa sasa ni moja kati ya timu bora nchini, ikiwa kwenye nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli amesema wanataka kwenda kwenye michuano ya kimataifa kwa nguvu zao wenyewe, hivyo wanaichukulia uzito mechi hiyo kwa sababu inaweza kuwapa nafasi ya kucheza mechi Kombe la Shirikisho Afrika.

Kocha wa Makipa wa timu hiyo, Razak Siwa, naye alisema wanahitaji kushinda mechi hiyo ili wawe kwenye nafasi nzuri ya kuiwakilisha nchi msimu ujao kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Huu ni mchezo muhimu, ni kama fainali, lengo ni kushiriki michuano ya kimataifa mwakani," alisema Siwa.

Lakini, Ofisa Habari wa Biashara United, Idrisa Sechambo, alisema wana uhakika wa kushinda mechi hiyo na kutinga fainali na kutwaa kombe hilo.

"Yanga ni saizi yetu, huwa tunawasumbua na hata ukiangalia michuano iliyopita walitutoa kwa penalti. Kwenye ligi pia tunawasumbua, tumejipanga kwenda fainali," alisema Sechambo.

Januari 31, 2019, katika michuano hiyo, Yanga ilitinga hatua ya 16-bora kwa mikwaju ya penalti 5-4 dhidi ya Biashara United baada ya matokeo ya mabao 2-2 ndani ya dakika 90 huku mwaka jana ikitolewa na watani zao, Simba hatua ya nusu fainali kwa kufungwa mabao 4-1.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Biashara United, Patrick Okumu, amesema wamejiandaa vema na mechi hiyo na kwa upande wao hawana majeruhi.

"Wachezaji wetu wana morali kubwa kucheza na Yanga. Najua utakuwa mchezo mgumu, lakini tumejiandaa vizuri," alisema kocha huyo raia wa Kenya.

Nahodha wa timu hiyo, Abdulmajid Mangalo, alisema: "Tukivuka hatua hii ni heshima kubwa sana kwetu, tunawaomba mashabiki wetu waje kwa wingi. Tutahakikisha tunawapa furaha ya kwenye fainali," alisema Mangalo.

## GOMES AFUNGUKA USAJILI MPYA SIMBA

**Na Saada Akida**

LICHA ya tetesi za usajili za Klabu ya Simba kuelekea msimu ujao kuzidi kugonga vichwa vya vyombo vya habari mbalimbali, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Didier Gomes amesema hataweka wazi nafasi alizopendekeza kusajiliwa nyota wapya kwa sasa kwa sababu hataki kuwavunja moyo wachezaji wake ndani ya kikosi hicho.

Akizungumza na gazeti hili jijini kabla ya kikosi cha timu hiyo kuelekea mjini Songea juzi tayari kwa mchezo wao wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho, maarufu FA Cup dhidi ya Azam FC, Gomes alisema hakuweka wazi mipango yake ya usajili kwa sababu bado wako katika mashindano.

Alisema hawezi kuweka wazi kwa sababu wanahitaji kufikia malengo yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA, hivyo hiki ni kipindi cha kuwatia moyo zaidi wachezaji wake.

"Ninawapenda sana wachezaji wangu, kuhusu tetesi za usajili hasa safu ya ushambuliaji bado hilo suala sio la kuweka wazi, najivunia waliopo katika kikosi, kwa sasa wananipa matokeo mazuri na sitaweza kuwavunja moyo na kuwakatisha tamaa.

"Kwa sababu bado tuko katika mashindano hatujafikia malengo yetu, kikubwa ni kwamba hakutakuwa na mabadiliko makubwa sana katika usajili wangu, hasa nitaangalia upungufu wa kikosi changu na kukiimarisha kidogo," alisema Gomes.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002